



TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA
JAMII ADILIFU NA YENYE UJUZI

MTAALA WA DARAJA YA JUU YA SHULE ZA UPILI

KISWAHILI

GREDI YA 11

OKTOBA, 2025

Toleo la Kwanza 2025

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtalaa huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

ISBN: 978-9914-43-086-8

Kimechapishwa na kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya

YALIYOMO

YALIYOMO	ii
MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA	iv
DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI KATIKA MTAALA WA KIUMILISI	vi
MATOKEO YA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI	vi
ORODHA YA MASOMO KATIKA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI	vii
MGAO WA VIPINDI KATIKA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI	viii
KAULI KIINI	ix
MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI KATIKA DARAJA YA JUU YA SHULE ZA UPILI	x
MUHTASARI WA MADA NA MADA NDOGO	xi
1.0: MAADILI KATIKA UZALISHAJI WA MAPATO	1
2.0: NJIA ZIFAAZO ZA UTATUZI WA MIGOGORO	9
3.0 KUKUZA UWEZO NA VIPAJI MBALIMBALI	20
4.0 USALAMA MAHALI PA KAZI	29
5.0: KUKABILIANA NA MABADILIKO KATIKA FAMILIA	38
6.0: KUTUMIA TEKNOLOJIA KUDHIBITI TAKA	48
7.0: UADILIFU KATIKA UONGOZI WA KIJAMII	57
8.0: UNYANYASAJI WA KIJINSIA	66

9.0: UTAMADUNI NA MSHIKAMANO WA KIJAMII	76
10.0: AFYA YA AKILI	84
MWONGOZO WA VIGezo NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA ULIOPEENDEKEZWA	94
MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI	106

MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA

Elimu nchini Kenya inatakiwa:

1. Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa

Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kutatua mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana. Mielekeo hii itawawezesha wanajamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia ukuaji wa taifa.

2. Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa

Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa taifa la Kenya kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.

a) Mahitaji ya kijamii

Elimu nchini Kenya lazima iwatayarisha vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mageuzi taratibu ya kijamii kutokana na maendeleo ya usasa yanayojitokeza kwa kasi. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kuwa na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko haya.

b) Mahitaji ya kiuchumi

Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na uwezo wa kibinafsi unaohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika humu nchini.

c) Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda

Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda. Kenya inatambua mabadiliko ya kasi ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunahitaji kuwa sehemu ya maendeleo haya ili mfumo wetu wa elimu ulenge kimakusudi maarifa, stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko yanayoendelea ulimwenguni.

3. Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza

Elimu inapaswa kuwezesha kutambua, kukuza na kuimarisha vipawa vya kila mmoja ili kuweza kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

iv

4. Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini

Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.

5. Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji

Usawa wa kijamii kwa mfano, usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa. Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zenye changamoto zitakazowawezesha kutoa huduma jumuishi za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.

6. Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya

Elimu inafaa kuwapa vijana uelewa wa tamaduni za kale na za sasa na nafasi yazo katika jamii ya kisasa. Watoto wanafaa kuambatanisha maadili ya tamaduni bora na mahitaji yanayobadilika kulingana na maendeleo yanayotokea ili kujenga jamii thabiti ya kisasa.

7. Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine

Kenya ni sehemu ya jamii ya kimataifa. Ni sehemu ya mtandao changamano unaotegemeana wa watu na mataifa. Kwa hivyo, elimu inapaswa kuwaelekeza vijana kukubali uanachama wa jamii hii ya kimataifa pamoja na majukumu na uwajibikaji, haki na manufaa ambayo yanatokana na uanachama huu.

8. Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira

Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Aidha, inafaa kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira na kuwaelekeza vijana kuthamini usafi wa mazingira.

v

DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI KATIKA MTAALA WA KIUMILISI

Daraja ya Juu ya Shule za Upili, ni kiwango cha nne cha Elimu ya Msingi katika Mtaala wa Kiumilisi (CBC) ambayo wanafunzi watajiunga nayo baada ya kumaliza Chekechea, Shule ya Msingi, na Shule ya Junia. Lengo kuu la Daraja ya Shule za Upili ni kuwapa wanafunzi uzoefu wa awali wa chuo kikuu au taaluma, ambapo wanafunzi wanapata fursa ya kuchagua mielekeo na nyanja wanazovutiwa nazo na walizoonyesha uwezo katika viwango vya awali. Daraja ya Juu ya Shule za Upili inajumuisha miaka mitatu ya masomo kwa wanafunzi walio kati ya umri wa miaka 16-18 na huweka msingi wa elimu ya juu zaidi, mafunzo ya kitaaluma, na ulimwengu wa kazi. Katika ruwaza ya Mtaala wa Kiumilisi, wanafunzi watakaohitimu katika kiwango hiki wanatarajiwa kuwa raia waliohusishwa, waliowezeshwa, na waadilifu walio tayari kushiriki katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya taifa.

Katika kiwango hiki, wanafunzi watajifunza masomo saba (7) kama yalivyopendekezwa na Kamati ya Rais ya Mageuzi ya Elimu (PWPER, 2023). Masomo haya yanajumuisha masomo manne ya lazima ambayo ni: English, Kiswahili, Essential Mathematics/Core Mathematics na Community Service Learning – CSL. Wanafunzi watachagua kati ya Core Mathematics (kwa wanafunzi wanaofuatilia mkondo wa STEM) na Essential Mathematics (kwa wanafunzi wanaofuatilia mikondo isiyo ya STEM). Wanafunzi watachagua masomo mengine matatu kulingana na chaguo la taaluma, vipaji, mapendeleo yao kwa somo fulani, na haiba zao, wakisaidiwa na mwalimu wao wa Daraja ya juu shule za upili.

MATOKEO YA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI

Kufikia mwisho wa Daraja ya Juu ya Shule za Upili, mwanafunzi aweze:

1. Kuwasiliana ipasavyo na kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika miktadha mbalimbali.
2. Kutumia maarifa ya kihisabati, kimantiki na uwazaji kina katika utatuzi wa matatizo.
3. Kutumia maarifa ya kimsingi ya utafiti na sayansi kudhibiti mazingira yake na kutatua matatizo.
4. Kutumia vizuri vipaji mbalimbali kwa ajili ya burudani, kujiendeleza kitaaluma, kielimu pamoja na kimafunzo.
5. Kudumisha tunu za kitaifa, kimaadili na kidini katika maisha ya kila siku.
6. Kutumia na kuendeleza mikakati ya matunzo ya kiafya katika maisha ya kila siku.
7. Kulinda, kuhifadhi na kuboresha mazingira kwa ajili ya uendeleu.
8. Kudhihirisha uraia wa kitaifa na wa kimataifa kwa ajili ya utangamano wa kindugu.
9. Kuonyesha uthamini wa tofauti za watu na tamaduni.
10. Kuonyesha uwajibikaji katika kushughulikia masuala mtambuko.

vi

JEDWALI 1: ORODHA YA MASOMO KATIKA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI

Core Subjects	Arts & Sports Science	Social Sciences	Science, Technology, Engineering & Mathematics (STEM)
1. English 2. Kiswahili/KSL 3. Core Mathematics/ Essential Mathematics 4. Community Service Learning (CSL)	5. Sports and Recreation 6. Music and Dance 7. Theatre and Film 8. Fine Arts	9. Literature in English 10. Indigenous Languages 11. Fasihi ya Kiswahili 12. Sign Language 13. Arabic 14. French 15. German 16. Mandarin Chinese 17. Christian Religious Education 18. Islamic Religious Education 19. Hindu Religious Education 20. Business Studies 21. History and Citizenship 22. Geography	23. Biology 24. Chemistry 25. Physics 26. General Science 27. Agriculture 28. Computer Studies 29. Home Science 30. Aviation 31. Building Construction 32. Electricity 33. Metalwork 34. Power Mechanics 35. Wood Technology 36. Media Technology 37. Marine and Fisheries Technology

Tanbihi

- a) Physical Education (PE) na Ujuzi wa Teknolojia na Mawasiliano (ICT skills) utatolewa kwa wanafunzi wote ili kuwezesha ujifunzaji na kufurahia.
- b) Kila shule itatoa Mpangilio wa Mafundisho ya Kidini (PPI) kwa ajili ya maendeleo ya kimaadili, kiimani na tabia njema za wanafunzi.
- c) Kutakuwa na somo moja kwa ajili ya usomaji wa kibinafsi au kwa makundi ili kudumisha maarifa na kuimarisha ujuzi katika maeneo yanayochaguliwa na wanafunzi.

Jedwali la 2, hapa chini linatoa mwongozo wa mgao wa vipindi katika Daraja ya Juu Shule za Upili.

vii

JEDWALI 2: MGAO WA VIPINDI KATIKA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI

SOMO	Vipindi Kwa Wiki (Dakika 40 kwa kipindi)
MASOMO YA LAZIMA 4	
1. English	5
2. Kiswahili	5
3. Physical Education (PE)	5
4. Community Service Learning (CSL)	3
Masomo ya Kuchagua/Hiari	
5. Chaguo la 1	5
6. Chaguo la 2	5
7. Chaguo la 3	5
* Physical Education	3
* ICT Skills	2
* PPI	1
* Learner Personal /Group Study	1
Jumla ya idadi ya vipindi	40

viii

KAULI KIINI

Somo la Kiswahili katika Daraja ya Juu ya Shule za Upili linaendeleza maarifa, ujuzi na stadi ambazo mwanafunzi amepata katika Shule ya Junia. Lengo kuu ni kumwezesha mwanafunzi kupanua uelewa na umilisi wake wa lugha ya Kiswahili, si tu kama somo, bali pia kama chombo cha kumwezesha kuyafahamu mazingira yake, kudumisha mahusiano yafaayo ya kijamii na kushirikiana na tamaduni anuwai. Somo hili linashughulikia stadi nne za lugha, Kusikiliza, Kuzungumza, Kusoma na Kuandika, pamoja na matumizi ya lugha ambayo yanajumuisha Sarufi na Isimujamii. Vipengele vilivyoshughulikiwa kama vile kuzungumza kwa kushawishi, kusikiliza na kujibu mjadala, kuzungumza kwa kupasha habari, na uzungumzaji husishi, miongoni mwa vingine, vinamwimarishia mwanafunzi stadi za kimawasiliano huku zikimkuzia stadi za karne ya ishirini na moja kama vile uwazaji kina na utatuzi wa matatizo. Mada ya Isimujamii nayo inampa mwanafunzi stadi za kutumia lugha ipasavyo katika miktadha mbalimbali ya kijamii, hivyo kumjengea umilisi wa kimsingi kama vile uraia. Kadhalika, somo hili linamkuzia mwanafunzi ubunifu, huku likimpa mbinu za kushirikiana na wenzake kitaifa na kimataifa.

Ujifunzaji wa Kiswahili katika kiwango hiki unalenga kumjengea mwanafunzi msingi wa taaluma atakayofuata katika vyuo vya kati na vyuo vikuu, na hapo hapo kumtayarisha kwa ulimwengu wa ajira. Shughuli mbalimbali za ujifunzaji kama vile mjadala, uzungumzaji wa papo kwa hapo, uandishi wa tungo amilifu kama vile ripoti na kumbukukumbu, pamoja na kushiriki katika kazimradi, hazichangii tu kumkuzia mwanafunzi ufasaha wa lugha, bali pia kumpa nafasi ya kujitathmini na kubaini ubora na udhaifu wake.

Kufikia mwisho wa kozi, mwanafunzi anatarajiwa kwamba atakuwa amefikia kiwango cha juu cha umahiri katika lugha ya Kiswahili. Somo hili linamtayarisha mwanafunzi kwa taaluma mbalimbali zikiwemo taaluma ya habari na mawasiliano, ufundishaji na sheria. Somo hili linamfungulia mwanafunzi fursa za ajira katika vyombo vya habari na nyanja nyingine kama vile ufundishaji, utafiti, uchaphishaji, sanaa, burdani, tafsiri na ukalimani. Umilisi wa lugha hii pia unachangia kufanikisha utoaji wa huduma katika taaluma nyingine kama vile udaktari na uhandisi ambazo zinamhitaji mtaalamu kutagusana na wateja wake kwa lugha wanayoelewa.

ix

MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI KATIKA DARAJA YA JUU YA SHULE ZA UPILI

Kufikia mwisho wa Daraja ya juu ya Shule ya Upili, mwanafunzi aweze:

1. kusikiliza kwa makini na kuitikia ipasavyo kwa Kiswahili katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano.
2. kujieleza ipasavyo kimaandishi na kimazungumzo kwa kuzingatia kanuni za lugha ya Kiswahili,
3. kuwasiliana ipasavyo katika miktadha mbalimbali ya kijamii,
4. kusoma kwa ufasaha na kufasiri matini mbalimbali zilizochapishwa na za kidijitali ili kupata ujumbe,
5. kutumia teknolojia ipasavyo katika ujifunzaji na mawasiliano ili kukuza ujuzi wa kidijitali,
6. kutumia maadili yanayohitajika maishani kupitia stadi za lugha ya Kiswahili,
7. kuonea fahari lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi, ya taifa na kimataifa.

x

MUHTASARI WA MADA NA MADA NDOGO

Mada	Mada Ndogo
Kusikiliza na Kuzungumza	1.1.1 Ufahamu wa Kusikiliza: <i>Ujumbe na fani katika matini elezi</i>
	2.1.1 Matamshi Bora: <i>Sauti /chw/ na /shw/; /jw/ na /njw/</i>
	3.1.1 Uzungumzaji elekezi
	4.1.1 Kusikiliza kwa Kupata Habari
	5.1.1 Kusikiliza kwa Kupambanua
	6.1.1 Uzungumzaji wa papo kwa hapo: <i>Muktadha wa sherehe</i>
	7.1.1. Kuzungumza kwa ufasaha: <i>Mjadala</i>
	8.1.1 Kuzungumza kwa kushawishi: <i>Ushawishi kuhusu maadili</i>
	9.1.1 Usikilizaji husishi: <i>Miktadha rasmi ya kikazi</i>
	10.1.1 Kusikiliza kwa Kuhakiki: <i>Muktadha usio rasmi</i>
Kusoma	1.2.1 Kusoma kwa Ufasaha: <i>Kifungu cha kupasha habari</i>
	2.2.1 Kusoma kwa Ufahamu: <i>Kifungu cha kupasha habari</i>
	3.2.1 Ufupisho: <i>Kifungu simulizi</i>

xi

Mada	Mada Ndogo
	4.2.1 Kusoma kwa Mapana: <i>Matini ya kujichagulia</i>
	5.2.1 Kusoma kwa Kina: <i>Usomaji wa kurashia</i>
	6.2.1 Kusoma kwa Ufasaha: <i>Kifungu cha mjadala</i>
	7.2.1 Kusoma kwa Ufahamu: <i>Kifungu cha kupasha habari</i>
	8.2.1 Ufupisho: <i>Kifungu shawishi</i>
	9.2.1 Kusoma kwa Mapana: <i>Matini ya kujichagulia</i>
	10.2.1 Kusoma kwa Kina: <i>Usomaji wa kuduhushi</i>
Kuandika	1.3.1 Viakifishi: <i>kiulizi (?), alama hisi (!), ritifaa ('), semi koloni/nukta mkato (;) na koloni/nukta pacha (:)</i>
	2.3.1 Uandishi wa Kiuamilifu: <i>Barua rasmi</i>
	3.3.1 Uandishi wa Kiuamilifu: <i>Tawasifu</i>
	4.3.1 Uandishi wa Kiuamilifu: <i>Memo</i>
	5.3.1: Uhariri: <i>Kuhariri Matini</i>
	6.3.1 Uandishi wa Kiuamilifu: <i>ripoti</i>

Mada	Mada Ndogo
	7.3.1 Uandishi wa Kiuamilifu: <i>Hotuba</i>
	8.3.1 Uandishi wa Kiubunifu: <i>Masimulizi kutokana na methali</i>
	9.3.1 Uandishi wa Kiuamilifu: <i>Insha fafanuzi kuhusu chanzo na athari</i>
	10.3.1 Tafsiri
Matumizi Ya Lugha	1.4.1 Aina za Maneno: <i>Aina za nomino na vivumishi</i>
	2.4.1 Ngeli za Nomino: <i>Ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA</i>
	3.4.1 Nyakati na Hali: <i>Hali -me-, hu-, -ka-</i>
	4.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi: <i>Tendatenda, tendeka, tendesha, tendana</i>
	5.4.1 Ukanushaji: <i>Hali ya -me-, hu-, -ka-</i>
	6.4.1 Aina za Maneno: <i>Aina za vitenzi na vielezi</i>
	7.4.1 Uundaji wa Maneno
	8.4.1 Mahusiano ya Kimaana: <i>Visawe vya nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi</i>
	9.4.1 Sentensi: <i>Sehemu za sentensi</i>
	10.4.1 Isimujamii: <i>Sajili za lugha</i>

1.0: MAADILI KATIKA UZALISHAJI WA MAPATO

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
1.1 Kusikiliza na Kuzungumza	1.1.1 Ufahamu wa Kusikiliza <i>Ujumbe na fani katika matini elezi</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kujadili maana ya ujumbe na fani katika matini ili kuvipambanua, b) kutabiri ujumbe katika matini elezi aliyosikiliza kwa kuzingatia anwani au picha, c) kutambua ujumbe katika matini elezi aliyosikiliza, d) kuchambua vipengele vya fani katika matini elezi aliyosikiliza, e) kuchangamkia kuchambua ujumbe na fani katika ufahamu wa kusikiliza ili kukuza stadi ya kusikiliza.	Mwanafunzi aelekezwe: - kujadili na wenzake maana ya ujumbe na fani katika matini, - kutoa utabiri kuhusu ujumbe wa matini elezi kwa kuzingatia anwani au picha, - kusikiliza matini elezi kuhusu suala lengwa kutoka kwa wenzake, mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali na kuthibitisha utabiri wake, - kutambua ujumbe katika matini elezi aliyosikiliza akishirikiana na wenzake, - kuchambua vipengele vya fani katika matini elezi aliyosikiliza (<i>k.v. mandhari, wahusika na matumizi ya lugha</i>) na kuwawasilishia wenzake kazi yake ili wamtotele maoni,	- Je, umewahi kusikiliza matini ipi elezi ili kuchambua ujumbe na fani? - Je, unazingatia nini ili kutambua ujumbe na fani katika matini elezi?

			kusikiliza matini elezi zaidi katika kifaa cha kidijitali na kuchambua ujumbe na fani.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili maana ya ujumbe na fani katika matini. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapofasiri ujumbe kutokana na matini elezi. Pia, anapochambua vipengele vya fani katika matini elezi. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kusikiliza matini elezi katika kifaa cha kidijitali na kuchambua ujumbe na fani.				
Maadili: - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kusikiliza matini elezi. - Heshima: Mwanafunzi anapowatolea wenzake maoni kuhusu uchambuzi wao wa vipengele vya fani katika matini elezi waliyosikiliza. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kutambua ujumbe na kuchambua vipengele vya fani katika matini elezi.				
Masuala Mtambuko: - Elimu ya kifedha: Mwanafunzi anaposikiliza matini elezi kuhusu suala lengwa (maadili katika uzalishaji wa mapato). - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusikiliza matini elezi na kuchambua ujumbe.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
1.2 Kusoma	1.2.1 Kusoma kwa Ufasaha <i>Kifungu cha kupasha habari</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kujadili vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa ufasaha ili kuvipambanua, b) kusoma kifungu cha kupasha habari akizingatia matamshi bora, c) kusoma kifungu cha kupasha habari akizingatia kasi ifaayo na kiwango kifaacho cha sauti, d) kusoma kifungu cha kupasha habari akizingatia viakifishi na kiimbo ipasavyo, e) kusoma kifungu cha kupasha habari akizingatia viziada lugha,	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza maana ya kifungu cha kupasha habari, - kutafiti katika mtandao salama kuhusu vipengele vya kusoma kwa ufasaha, - kujadili vipengele vya kusoma kifungu cha kupasha habari (<i>k.v. kuzingatia ujumbe, matamshi bora, kiwango kifaacho cha sauti, kasi ifaayo, kiimbo, viakifishi na viziada lugha</i>) akishirikiana na wenzake, - kusoma kifungu cha kupasha habari kuhusu suala lengwa kwenye vitabu, magazeti, majarida au kwenye kifaa cha kidijitali akizingatia matamshi bora, kiwango kifaacho cha sauti, kasi ifaayo, kiimbo, viakifishi na viziada lugha vifaavyo akishirikiana na wenzake, - kusoma kifungu cha kupasha habari kwa ufasaha na kujirekodi kwenye kifaa cha kidijitali, - kuwasambazia wenzake mtandaoni kifungu alichojirekodi akisoma ili	- Unazingatia nini ili uweze kusoma kifungu cha kupasha habari kwa ufasaha? - Usomaji wa kifungu cha kupasha habari kwa ufasaha una umuhimu gani katika mawasiliano?

		f) kuchangamkia kusoma kifungu cha kupasha habari akizingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano.	wakitathmini na kumtolea maoni kwa heshima, kutafiti vifungu vya kupasha habari kwenye mtandao salama na kuvisoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya kusoma kifungu cha kupasha habari. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapotafiti vifungu vya kupasha habari mtandaoni na kuvisoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapojirekodi kwenye kifaa cha kidijitali na kuwasambazia wenzake ili wamtotee maoni.				
Maadili: - Heshima: Mwanafunzi anapowatolea wenzake maoni kuhusu usomaji wao. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma kifungu cha kupasha habari wakizingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha.				
Masuala Mtambuko: - Elimu ya kifedha: Mwanafunzi anaposoma kifungu cha kupasha habari kuhusu suala lengwa la maadili katika uzalishaji wa mapato. - Usalama wa mtandaoni: Mwanafunzi anaposoma kifungu cha kupasha habari kwa kuzingatia maadili ya mtandaoni.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Swali Dadisi Linalopendekezwa
1.3 Kuandika	1.3.1 Viakifishi - <i>Kiulizi</i> - <i>Alama ya hisi</i> - <i>Ritifaa</i> - <i>Semi koloni/nukta mkato</i> - <i>Koloni/nukta pacha</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza matumizi ya kiulizi, alama ya hisi, ritifaa, semi koloni na koloni katika matini ili kuyatofautisha, b) kutumia ipasavyo kiulizi, alama ya hisi, ritifaa, semi koloni na koloni katika matini, c) kujenga mazoea ya kutumia alama za uakifishi ipasavyo katika matini ili kufanikisha mawasiliano.	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza matumizi ya kiulizi, alama ya hisi, ritifaa, semi koloni na koloni, - kusakura mtandao salama kuhusu matumizi ya kiulizi, alama ya hisi, ritifaa, semi koloni na koloni akishirikiana na wenzake, - kuandika kwenye chati matumizi ya kiulizi, alama ya hisi, ritifaa, semi koloni na koloni na kuitundika ukutani akishirikiana na wenzake, - kusahihisha sentensi au vifungu vifupi ambavyo havijatumiwa ipasavyo kiulizi, alama ya hisi, ritifaa, semi koloni na koloni, - kutunga sentensi au kifungu kifupi kwa kuzingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala lengwa akitumia kiulizi, alama ya hisi, ritifaa, semi koloni na koloni ipasavyo, - kuwasilisha sentensi au kifungu kifupi alichotunga darasani ili wenzake wamtotee maoni kwa heshima na upendo.	Kwa nini alama za uakifishi ni muhimu katika maandishi?

Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni kuhusu matumizi ya viakifishi lengwa. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapoeleza ipasavyo matumizi ya viakifishi lengwa. - Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga sentensi au kifungu kifupi akizingatia matumizi yafaayo ya viakifishi lengwa.
Maadili: - Uwajibikaji: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni na kuandika kuhusu matumizi ya viakifishi lengwa. - Heshima: Mwanafunzi anaposikiliza na kuthamini maoni ya wenzake akieleza matumizi ya alama lengwa za uakifishi. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika alama za uakifishi kwenye chati. - Upendo: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.
Masuala Mtambuko: - Elimu ya kifedha: Mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa. - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujifunza jinsi ya kutumia kanuni za uakifishi.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
1.4 Matumizi ya Lugha	1.4.1 Aina za Maneno <i>Aina za:</i> - <i>Nomino</i> - <i>Vivumishi</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kujadili aina mbalimbali za nomino na vivumishi ili kuvibainisha, b) kutambua aina za nomino na vivumishi katika tungo, c) kutumia aina za nomino na vivumishi katika matini, d) kuchangamkia matumizi ya aina za nomino na vivumishi ili kujenga ufasaha wa lugha.	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza maana ya nomino na vivumishi, - kutaja mifano ya nomino na vivumishi akishirikiana na wenzake, - kujadili aina mbalimbali za nomino na vivumishi akishirikiana na wenzake, - kusoma vitabuni au kusakura mtandao salama kuhusu aina za nomino na vivumishi akishirikiana na wenzake, - kudondoa aina za nomino (<i>k.v. pekee, kawaida na dhahania</i>) na vivumishi (<i>k.v. vimilikishi, viashiria na sifa</i>) katika kundi la maneno, - kutambua aina za nomino na vivumishi katika sentensi au vifungu vifupi, - kujaza nafasi katika sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia aina za nomino na vivumishi ipasavyo, - kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia aina za nomino na	- Je, unajua aina zipi za nomino na vivumishi? - Je, ni mambo gani yanayosababisha kuwepo kwa aina mbalimbali za nomino na vivumishi?

			vivumishi akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala lengwa, kuwawasilishia wenzake sentensi na vifungu vifupi alivyotunga ili wamtolee maoni kwa heshima.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kuhusu aina za nomino na vivumishi. - Kujiamini: Mwanafunzi anapotunga sentensi na vifungu vifupi kwa usahihi na kuwawasilishia wenzake ili wamtolee maoni kwa heshima. - Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga sentensi na vifungu vifupi kwa usahihi akitumia aina za nomino na vivumishi. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anaposoma vitabu au kusakura mtandaoni ili kutambua aina za nomino na vivumishi.				
Maadili: - Amani: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu na kuelewana wanapojadili kuhusu aina za nomino na vivumishi. - Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu sentensi na vifungu vifupi alivyotunga na kuwasilishia. - Umoja: Mwanafunzi anaopojumuika na wenzake na kutambua aina za nomino na vivumishi. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapovitunza vifaa vya kidijitali kusakura mtandaoni kuhusu aina za nomino. Pia, anaposhiriki kikamilifu katika shughuli za ujifunzaji.				
Masuala Mtambuko: - Elimu ya kifedha: Mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa akitumia aina za nomino na vivumishi. - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua aina za nomino na vivumishi katika matini. - Mawasiliano bora: Mwanafunzi anapowawasilishia wenzake sentensi na vifungu vifupi alivyotunga.				

2.0: NJIA ZIFAAZO ZA UTATUZI WA MIGOGORO

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
2.1 Kusikiliza na Kuzungumza	2.1.1 Matamshi Bora <i>Sauti</i> - /chw/ na /shw/ - /jw/ na /njw/	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kutambua maneno yenye sauti /chw/ na /shw/, na /jw/ na /njw/ katika matini, b) kutamka maneno yenye sauti /chw/ na /shw/, na /jw/ na /njw/ ipasavyo katika maneno, c) kutamka vitanzandimi vyenye sauti /chw/ na /shw/, na /jw/ na /njw/ ipasavyo, d) kutunga vitanzandimi vyenye sauti /chw/ na /shw/, na /jw/ na /njw/ ipasavyo, e) kuchangamkia matumizi ya sauti /chw/ na /shw/, na /jw/ na /njw/ katika	Mwanafunzi aelekezwe: • kutambua maneno yenye sauti /chw/ na /shw/, na /jw/ na /njw/, katika chati au kadi za maneno akishirikiana na wenzake, • kusikiliza kifungu chenye maneno yenye sauti /chw/ na /shw/, na /jw/ na /njw/, kwenye kifaa cha kidijitali na kuzitambua, • kutambua maneno yenye sauti /chw/ (k.v. <i>mchwa, kichwa, chwara</i>), /shw/ (k.v. <i>shwari, oshwa, wishwa</i>), /jw/ (k.v. <i>fujwa, chujwa</i>), na /njw/ (k.v. <i>ugonjwa, kunjwa na vunjwa</i>) katika matini akishirikiana na wenzake, • kutamka maneno yenye sauti /chw/ na /shw/, na /jw/ na /njw/, ipasavyo katika nyenzo kama vile kadi za maneno akishirikiana na wenzake,	1. Je, ni vifaa au hali gani katika mazingira yako ambazo zina majina yenye sauti /chw/ na /shw/, na /jw/ na /njw/? 2. Kwa nini ni muhimu kutamka maneno ipasavyo tunapowasiliana? 3. Ni mambo gani yanayoweza kukufanya usitamke maneno vizuri?

		mawasiliano ili kukuza matamshi bora.	- kutathmini matamshi ya mwenzake ya maneno yenye sauti /chw/ na /shw/, na /jw/ na /njw/ kwa heshima na upendo, - kutamka vitanzandimi vyenye maneno ya sauti /chw/ na /shw/, na /jw/ na /njw/ ipasavyo, - kutunga vitanzandimi vyenye maana kwa kutumia maneno yenye sauti /chw/ na /shw/, na /jw/ na /njw/, - kujirekodi akitamka harakaharaka vitanzandimi alivyotunga, - kuwachezea wenzake rekodi ya vitanzandimi alivyovitunga au kuwatamkia vitanzandimi hivyo ili wavitolee maoni kwa heshima.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusikiliza kifungu na kutambua maneno yenye sauti lengwa. - Kujiamini: Mwanafunzi anapotamka maneno yenye sauti lengwa ipasavyo. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotamka vitanzandimi na kujirekodi katika kifaa cha kidijitali. - Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga vitanzandimi kwa kutumia maneno yenye sauti lengwa.				

Maadili:

- Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Heshima: Mwanafunzi anapowatolea wenzake maoni kwa heshima kuhusu namna walivyotamka maneno yenye sauti lengwa.
- Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujirekodi akitamka sauti lengwa. Pia, anaposhiriki kikamilifu katika shughuli za ujifunzaji.

Masuala Mtambuko:

- Utatuzi wa migogoro: Mwanafunzi anapotumia njia za amani kusuluhisha kutoelewana kunakoweza kutokea anaposhirikiana na wenzake kusikiliza na kutamka sauti lengwa.
- Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Suala la teknolojia katika elimu na maendeleo: Mwanafunzi anapojirekodi akitamka vitanzandimi na kuwachezea wenzake.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
2.2 Kusoma	2.2.1 Kusoma kwa Ufahamu <i>Kifungu cha kupasha habari</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza habari mahususi katika kifungu cha kupasha habari, - kupanga matukio yanavyofuatana katika kifungu cha kupasha habari alichosoma, - kufanya utabiri na ufasiri kutokana na kifungu cha kupasha habari, - kutumia msamiati kutoka kifungu cha kupasha habari ipasavyo katika sentensi au kifungu kifupi, - kujenga mazoea kusoma kifungu cha ufahamu ili	Mwanafunzi aelekezwe: - kusoma kifungu cha kupasha habari kuhusu suala lengwa kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali, - kujadili habari mahususi (<i>k.v. nani, nini, wapi, lini na kwa nini</i>) katika kifungu cha kupasha habari akishirikiana na wenzake, - kupanga matukio yanavyofuatana katika kifungu cha kupasha habari akishirikiana na wenzake huku wakitolea maoni kwa heshima, - kufanya utabiri na ufasiri kutokana na kifungu cha kupasha habari alichokisoma, - kutambua msamiati (<i>k.v. maneno na nahau</i>) katika kifungu cha kupasha habari na kueleza maana kimuktadha au kwa kutumia kamusi, - kutunga sentensi au kifungu kifupi akitumia msamiati alioutambua katika kifungu cha kupasha habari ipasavyo,	- Je, umewahi kusoma kifungu kipi cha kupasha habari? - Je, utazingatia nini ili kupata ujumbe katika kifungu cha kupasha habari?

		kukuza uelewa wa habari.	kusoma vifungu zaidi vya kupasha habari kwenye vitabu au katika vifaa salama vya kidijitali kuhusu suala lengwa kisha aeleze maana za misamiati.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji na kuchangia ipasavyo katika kupanga matukio kwenye kifungu. - Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia msamiati aliojifunza katika kifungu cha kupasha habari. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapofanya utabiri na kufasiri kuhusu kifungu cha kupasha habari.				
Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kutabiri na kufasiri kifungu cha kupasha habari. - Heshima: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kupanga matukio katika kifungu cha kupasha habari kwa kuthamini maoni yao.				
Masuala Mtambuko: - Utatuzi wa migogoro: Mwanafunzi anapojifunza kutokana na ujumbe wa kifungu alichosoma kuhusu suala lengwa. - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yanayopendekezwa
2.3 Kuandika	2.3.1 Uandishi wa Kiuamilifu <i>Barua rasmi</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza maana ya barua rasmi ili kuitofautisha na aina nyingine za barua, - kutambua miktadha ambapo barua rasmi huandikwa, - kueleza umuhimu wa barua rasmi katika mawasiliano, - kujadili vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa barua rasmi, - kuandika barua rasmi kwa kuzingatia vipengele vifaavyo, - kujenga mazoea ya kuandika barua	Mwanafunzi aelekezwe: - kushirikiana na wenzake kueleza maana ya barua rasmi, - kutafiti kwenye mtandao salama au vitabuni kuhusu aina za barua rasmi (<i>k.v. mialiko, kuomba kazi, kujibu mialiko, barua kwa mhariri</i>), - kujadili na kutambua miktadha ambapo barua rasmi huandikwa (<i>k.v. kuomba kazi, kualika kwenye sherehe au mkutano na kuomba msamaha</i>), - kufafanua umuhimu wa barua rasmi akishirikiana na wenzake, - kutafiti vitabuni au kwenye mtandao salama kuhusu vipengele vya kuzingatia katika kuandika barua rasmi (<i>ujumbe, muundo na mtindo</i>) na kuvijadili akishirikiana na wenzake, - kusoma vielelezo vya barua rasmi katika vitabu au vifaa vya kidijitali kwa uangalifu akishirikiana na wenzake ili kutambua vipengele vilivyozingatiwa,	- Je, umewahi kuandika barua rasmi kuhusu nini? - Je, ni kwa nini barua rasmi huandikwa?

		rasmi kwa kuzingatia vipengele vifaavyo ili kufanikisha mawasiliano.	- kuorodhesha hoja ambazo atatumia kuandika barua rasmi, - kuandika barua rasmi inayorejelea utatuzi wa migogoro kwa kuzingatia vipengele vyake, - kuwasomea wenzake barua rasmi aliyoandika ili watoe maoni.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapowasiliana na kushirikiana na wenzake kueleza maana ya barua rasmi. - Ubunifu: Mwanafunzi anapoandika barua rasmi kwa kuzingatia vipengele vifaavyo. - Kujiamini: Mwanafunzi anapofanikiwa kuandika barua rasmi na kuwasomea wenzake. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni kupata habari kuhusu vipengele vya barua rasmi. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapoorodhesha hoja ambazo atatumia kuandika barua rasmi.				
Maadili: - Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapojadili vipengele vya barua rasmi. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotunza na kuvitumia vifaa vya kidijitali. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusakura vipengele vya barua rasmi mtandaoni.				
Masuala Mtambuko: - Utatuzi wa migogoro: Mwanafunzi anapotatua ipasavyo tofauti za kimaoni na wenzake wanapojadili vipengele vya barua rasmi. - Usalama katika mtandao: Mwanafunzi anapotalii mtandao salama kutafuta vipengele vya kuzingatia katika kuandika barua rasmi.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
2.4 Matumizi ya Lugha	2.4.1 Ngeli za Nomino <i>Ngeli ya:</i> - I-I - U-ZI - LI-YA - LI-LI - YA-YA	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza dhana ya upatanisho wa kisarufi ili kuipambanua, - kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi katika ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA katika matini, - kujadili sifa za nomino za ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA ili kuzipambanua, - kutambua nomino za ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA katika matini, - kutumia nomino katika ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA katika matini kwa kuzingatia	Mwanafunzi aelekezwe: - kufafanua dhana ya upatanisho wa kisarufi, - kutaja viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA, - kutambua nomino za ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA katika matini (andishi au ya kidijitali) - kutafiti katika vitabu au kwenye mtandao salama sifa za nomino za ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA (<i>k.v. ngeli ya LI-YA hujumuisha majina yanayoanza kwa ji, katika umoja na ma/me katika wingi. Mifano: jina - majina, jicho- macho; hujumuisha majina ambayo hayachukui kiambishi katika umoja, lakini huwa na kiambishi ma katika wingi. Mfano: yai-</i>	- Tunawezaje kutambua nomino za ngeli mbalimbali? - Ni mambo gani tunayozingatia katika upatanisho wa kisarufi katika sentensi?

		upatanisho ufao wa kisarufi, f) kuonea fahari matumizi ya nomino za ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA ipasavyo katika sentensi na vifungu ili kuimarisha mawasiliano.	<i>mayai, shamba-mashamba)</i> akishirikiana na wenzake, - kujadili matokeo ya utafiti wake kuhusu sifa za nomino za ngeli lengwa, - kutenga nomino za ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA katika orodha yenye mchanganyiko wa nomino, - kutafiti nomino za ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA vitabuni au mtandaoni akishirikiana na wenzake, - kutunga sentensi au vifungu vifupi kuhusu masuala mtambuko anuwai, likiwemo suala lengwa, akizingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA, - kubadilisha nomino katika ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA kutoka hali ya umoja hadi hali ya wingi akishirikiana na wenzake, - kubadilisha sentensi zenye nomino za ngeli ya I-I, U-ZI, LI-	
--	--	---	---	--

			YA, LI-LI na YA-YA kutoka umoja hadi wingi na wingi hadi umoja, - kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia upatanisho wa kisarufi katika ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA ipasavyo, - kutunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA, akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala lengwa, - kuandika sentensi alizotunga kwenye chati na kuangika ukutani ili wenzake wazitolee maoni, - kuandika sentensi alizotunga kwenye kifaa cha kidijitali kwa uangalifu na kuwasambazia wenzake.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga sentensi na kuonyesha upatanisho ufao wa kisarufi. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutafiti kuhusu nomino za ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA vitabuni au mtandaoni.				

Kujiamini: Mwanafunzi anapofanikiwa kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI na YA-YA ipasavyo.
Maadili: - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotunza na kutumia kifaa cha kidijitali kutafiti nomino za ngeli lengwa. - Heshima: Mwanafunzi anapothamini mchango wa wenzake wanapobadilisha nomino za ngeli husika kutoka hali ya umoja hadi wingi. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutafiti nomino za ngeli lengwa vitabuni au mtandaoni.
Masuala Mtambuko: - Utatuzi wa migogoro: Mwanafunzi anapotunga sentensi zinazohusiana na suala lengwa. - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. - Mawasiliano bora: Mwanafunzi anapotunga sentensi akizingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ufao.

3.0 KUKUZA UWEZO NA VIPAJI MBALIMBALI

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
3.1 Kusikiliza na Kuzungumza	3.1.1 Uzungumzaji Elekezi <i>(Maelezo sahihi, angavu na yenye mvuto kuhusu mahali, hali na vitu)</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza maana ya uzungumzaji elekezi ili kuotofautisha na aina nyingine za uzungumzaji, - kujadili umuhimu wa uzungumzaji elekezi, - kujadili vipengele vya kuzingatia katika uzungumzaji elekezi kuhusu mahali, hali na vitu, - kutambua uzungumzaji elekezi kuhusu mahali, hali na vitu miongoni mwa aina mbalimbali za	Mwanafunzi aelekezwe: - kutafiti kuhusu maana ya uzungumzaji elekezi, - kushirikiana na wenzake kujadili miktadha ambapo uzungumzaji elekezi hutokea (<i>k.v. kuelekeza kuhusu mienendo, kuhusu namna ya kutambua na kukuza talanta, kuhusu namna ya kutumia mitambo fulani</i>), - kujadili na wenzake umuhimu wa uzungumzaji elekezi, - kutafiti kwenye vitabu au mtandao salama vipengele vya kuzingatia katika kutoa uzungumzaji elekezi kuhusu mahali, hali na vitu: usahihi (<i>k.v. ujumbe kugonga ndipo na ukweli unaotolewa panapofaa</i>), uangavu (<i>k.v. lugha fasaha, msamiati unaoeleweka, mtiririko, toni, matamshi sahihi</i>)	- Je, umewahi kushiriki katika uzungumzaji elekezi katika miktadha gani? - Kwa nini ni muhimu kutoa mazungumzo ya kuelekeza kuhusu mahali, hali na vitu? - Ni mambo gani tunafaa kuzingatia ili kufanikisha mazungumzo ya kuelekeza kuhusu mahali, hali, na vitu?

		uzungumzaji alizosikiliza, e) kuwasilisha mazungumzo elekezi kuhusu mahali, hali na vitu kwa kuzingatia vipengele vifaavyo, f) kujenga mazoea ya kuzungumza kwa kuelekeza kwa kuzingatia vipengele vyake ili kufanikisha mawasiliano.	na mvuto (k.v. kutumia <i>lugha inayomjengea msikilizaji taswira ya mahali au kitu anachotoa habari kuhusu, kushirikisha hadhira, matumizi ya viziada lugha, tamathali za usemi</i>) akishirikiana na wenzake, • kusikiliza aina mbalimbali za uzungumzaji kutoka kwa wanafunzi wenzake, mwalimu, mgeni mwalikwa, au vifaa vya kidijitali na kutambua uzungumzaji elekezi kuhusu mahali, hali na vitu, • kuwasilisha darasani mazungumzo ya kuelekeza kuhusu mahali na vitu kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uzungumzaji wa aina hii na suala lengwa, • kusikiliza mazungumzo elekezi ya wenzake na kuyatolea maoni kwa heshima.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kuhusu miktadha ambapo uzungumzaji elekezi hutokea na umuhimu wake.				

- Ubunifu: Mwanafunzi anapotumia vipengele anuwai kuwasilisha uzungumzaji elekezi kuhusu mahali, hali na vitu darasani. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni kuhusu vipengele vya uzungumzaji elekezi kuhusu mahali, hali na vitu. - Kujiamini: Mwanafunzi anapofanikiwa kuwasilisha mazungumzo elekezi darasani.
Maadili: - Heshima: Mwanafunzi anaposikiliza na kuthamini mazungumzo ya wenzake. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya uzungumzaji elekezi kuhusu mahali, hali na vitu.
Masuala Mtambuko: - Ukuzaji wa vipaji: Mwanafunzi anapowasilisha mazungumzo elekezi kuhusu mahali, hali na vitu darasani akizingatia suala lengwa. - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuwasilisha mazungumzo elekezi habari kuhusu mahali, hali na vitu mbalimbali katika jamii mahususi.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Swali Dadisi Lililopendekezwa
3.2 Kusoma	3.2.1 Ufupisho <i>Kifungu Simulizi</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya ufupisho ili kuupambanua, b) kutambua miktadha ya kijamii ambapo ufupisho hufanyika, c) kujadili vipengele vya kuzingatia katika kufupisha kifungu simulizi, d) kufupisha kifungu simulizi kwa kuzingatia vipengele vya ufupisho, e) kuchangamkia usomaji wa matini mbalimbali kwa nia ya kuyafupisha bila kupoteza ujumbe kusudiwa.	Mwanafunzi aelekezwe: - kushirikiana na wenzake kujadili maana ya ufupisho, - kujadili miktadha ya kijamii ambapo ufupisho wa vifungu hutumika, - kutafiti kwa mtandao salama au maktabani vipengele vya kuzingatia katika kufupisha kifungu simulizi, - kushirikiana na wenzake kusoma vielelezo vya vifungu simulizi mbalimbali vilivyofupishwa ili kutambua namna ya kuvifupisha, - kusoma vifungu simulizi na kuvifupisha kwa kuzingatia vipengele vya ufupisho, - kuwasilisha ufupisho wake darasani ili wenzake wautolee maoni kwa heshima na upendo.	Ufupisho wa kifungu simulizi una umuhimu gani?
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili maana ya ufupisho.				

- Kujiamini: Mwanafunzi anapofaulu kufupisha kifungu simulizi na kuwawasilishia wenzake. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapotafakari kuhusu hoja za kudondoa katika kifungu simulizi.
Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili maana ya ufupisho. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotafiti katika mtandao salama vipengele vya kuzingatia katika kufupisha kifungu. - Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake anapowasilisha ufupisho wake darasani.
Masuala Mtambuko: - Ukuzaji wa vipaji mbalimbali: Mwanafunzi anaposoma na kufupisha kifungu kuhusu suala lengwa. - Mtazamo wa ukuaji wa binadamu: Mwanafunzi anapogundua kipawa na uwezo wake anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Swali Dadisi Lililopendekezwa
3.3 Kuandika	3.3.1 Uandishi wa Kiuamilifu <i>Tawasifu</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya insha ya tawasifu, b) kujadili vipengele vya insha ya tawasifu, c) kuandika insha ya tawasifu kwa kuzingatia vipengele vyake, d) kufurahia kuandika insha za tawasifu ili kukuza ubunifu.	Mwanafunzi aelekezwe: • kueleza maana ya insha ya tawasifu akishirikiana na wenzake, • kujadili ujumbe wa insha ya tawasifu akishirikiana na wenzake, • kujadili muundo wa insha ya tawasifu (<i>k.v. aya zenye kubainisha utangulizi, mwili na hitimisho</i>) akishirikiana na wenzake, • kujadili mtindo wa insha ya tawasifu (<i>k.v. msamiati mwafaka, tamathali za usemi, lugha sanifu na mtiririko ufaao</i>) akishirikiana na wenzake, • kusoma kielelezo cha tawasifu mtandaoni au maktabani akiwa na mwenzake, • kuandika insha ya tawasifu kuhusu suala lengwa akizingatia ujumbe, muundo na mtindo ufaao, • kutumia kifaa cha kidijitali kuwasambazia wenzake insha ya tawasifu aliyoandika,	Insha ya tawasifu ina umuhimu gani?

			kuwasomea wenzake darasani insha ya tawasifu aliyoandika.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapojadili na wenzake kuhusu vipengele vya insha ya tawasifu. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kuwasambazia wenzake insha ya tawasifu aliyoandika. - Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga insha ya tawasifu kuhusu suala lengwa. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapobuni hoja za ujumbe wa insha ya tawasifu. - Kujiamini: Mwanafunzi anapofaulu kuandika na kuwawasilishia insha ya tawasifu ifaavyo.				
Maadili: - Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu muundo na ujumbe wa insha ya tawasifu. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili muundo na ujumbe wa insha ya tawasifu. - Upendo: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu kujadili maana na mtindo wa insha ya tawasifu.				
Masuala Mtambuko: - Utambuzi wa vipaji na uwezo: Mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa. - Mtazamo wa ukuaji wa binadamu: Mwanafunzi anapoandika tawasifu akiangazia kipaji chake.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Swali Dadisi Lilibendekezwa
3.4 Matumizi ya Lugha	3.4.1 Nyakati na Hali Hali ya: -me- -hu- -ka-	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kubainisha vitenzi vilivyo katika hali ya -me-, hu- na -ka- katika matini, b) kutumia hali ya -me-, hu- na -ka- ifaavyo katika matini, c) kuchangamkia ufasaha wa lugha kwa kutumia hali ya -me-, hu-, na -ka- ifaavyo katika mawasiliano.	Mwanafunzi aelekezwe: - kutaja hali mbalimbali (k.v. -me-, hu- na -ka-), - kutambua viambishi vya hali ya -me-, hu- na -ka- katika matini akiwa na wenzake, - kutambua vitenzi vilivyo katika hali ya -me-, hu- na -ka- kwenye matini kama vile chati akishirikiana na wenzake, - kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia hali ya -me-, hu- na -ka- ipasavyo, - kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia hali ya -me-, hu- na -ka- akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la kukuza uwezo na vipaji mbalimbali, - kuwawasilishia wenzake sentensi na vifungu alivyotunga ili watoe maoni yao kwa heshima.	Je, ni hali zipi zinazoonyesha kutendeka kwa vitendo?

Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na mwenzake kutambua viambishi vya hali mbalimbali katika matini. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandikia sentensi na kuwasambazia wenzake ili watoe maoni. - Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga sentensi katika hali ya -me-, hu- na -ka-. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapotambua hali lengwa kwenye vitenzi. - Kujiamini: Mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia hali lengwa kwa njia sahihi.
Maadili: - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapoandika sentensi akitumia hali ya -me-, hu- na -ka- na kutunza vifaa vya kidijitali. - Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu sentensi alizotunga akitumia hali lengwa. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana kwa amani na wenzake katika kutambua viambishi vya hali ya -me-, hu- na -ka- katika matini.
Masuala Mtambuko: - Ukuzaji wa vipaji: Mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa. - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. - Mawasiliano bora: Mwanafunzi anapotunga sentensi na kuwawasilishia wenzake akitumia hali lengwa ipasavyo.

4.0 USALAMA MAHALI PA KAZI

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
4.1 Kusikiliza na Kuzungumza	4.1.1 Kusikiliza kwa Kupata Habari <i>Kumbukumbu na maamuzi</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kujadili vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa kupata habari ili kukuza kumbukumbu na maamuzi, b) kusikiliza mazungumzo akizingatia vipengele vya kusikiliza kwa kupata habari, ili kukuza kumbukumbu na maamuzi, c) kuchanganua mitazamo na mielekeo ya ujumbe katika matini aliyosikiliza, d) kutoa muhtasari wa ujumbe katika matini	Mwanafunzi aelekezwe: - kujadili vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa kupata habari ili kukuza kumbukumbu (k.v. <i>kusikiliza kwa makini, kumtazama msemaji moja kwa moja, kuuliza maswali, kurudia baadhi ya hoja akilini, kuchunguza ishara za uso na mwili na kutoa muhtasari</i>) na maamuzi (<i>kutafakari kuhusu yanayosemwa, kuzingatia toni na kiimbo, kuwa na mtazamo wazi usio nafsi, kuchunguza ishara za uso na mwili</i>) akishirikiana na wenzake, - kuandika kwenye chati, vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa kupata habari kwa nia ya kukumbuka na	- Je, kusikiliza habari kwa makini kunasaidiaje kukuza kumbukumbu kuhusu ujumbe wa habari hiyo? - Je, ni mambo gani utakayozingatia unaposikiliza habari ili uweze kutoa maamuzi yafaayo kuhusu mtazamo na mwelekeo wa ujumbe wa habari hiyo?

		aliyosikiliza ili kukuza kumbukumbu, e) kujenga mazoea ya kuzingatia kanuni zifaazo za kusikiliza kwa kupata habari ili kuimarisha usikilizaji.	kufanya maamuzi na kuvitundika ukutani akishirikiana na wenzake, - kusikiliza habari au maelezo kuhusu suala lengwa kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye kifaa cha kidijitali akizingatia vipengele vifaavyo, - kusikiliza matini kuhusu suala lengwa kutoka kwa mwalimu au mgeni mwalikwa na kujadili mitazamo na mielekeo ya ujumbe akishirikiana na wenzake, - kuwasilishia wenzake ujumbe wa matini aliyosikiliza ili watathmini kumbukumbu yake, - kusikiliza matini kuhusu suala lengwa kutoka kwa mwalimu au mgeni mwalikwa na kujadili mitazamo na mielekeo ya ujumbe akishirikiana na wenzake, - kushiriki mazungumzo akizingatia vipengele vya	
--	--	---	---	--

			kusikiliza kwa kupata habari vinavyokuza kumbukumbu na uwezo wa kutoa maamuzi akiwa na wenzake.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kupata habari kuhusu vipengele vya kusikiliza kwa kupata habari ili kukuza kumbukumbu na maamuzi. • Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapotafakari na kutoa maamuzi kuhusu mitazamo na mielekeo ya ujumbe. • Kujiamini: Mwanafunzi anapofanikiwa kuwawasilishia wenzake ujumbe aliopata katika matini aliyosikiliza.				
Maadili: • Uwajibikaji: Mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu katika shughuli za ujifunzaji. Pia anapotunza vifaa vya kidijitali. • Heshima: Mwanafunzi anapothamini kumbukumbu ya wenzake. • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusikiliza matini kwa kuzingatia vipengele vya usikilizaji vinavyoweza kukuza kumbukumbu na kutoa maamuzi kuhusu ujumbe. • Amani: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusikiliza matini kwa utulivu.				
Masuala Mtambuko: • Suala la usalama: Mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo kuhusu suala lengwa akizingatia vipengele vya usikilizaji vinavyokuza kumbukumbu na uwezo wa kutoa maamuzi. • Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili mitazamo na mielekeo ya ujumbe wa matini waliosikiliza.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
4.2 Kusoma	4.2.1 Kusoma kwa Mapana <i>Matini ya kujichagulia</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kujadili vipengele mbalimbali vya kuzingatia katika kusoma kwa mapana, b) kusoma matini ya kujichagulia akizingatia msamiati na matumizi ya lugha, c) kuandika muhtasari wa ujumbe wa matini aliyoisoma, d) kufurahia kusoma kwa mapana ili kujenga ufasaha wa lugha.	Mwanafunzi aelekezwe: • kujadili vipengele vya kusoma kwa mapana (<i>kutambua msamiati, kutambua ujumbe na kuandika muhtasari wa matini</i>) akishirikiana na wenzake, • kutambua matini ya kujichagulia (<i>andishi au ya kidijitali</i>) kuhusu suala lengwa au suala lolote linaloathiri jamii na kuisoma, • kutumia kamusi kutafuta maana za maneno asiyoyajua, • kuandika msamiati aliojifunza na maana yake daftarinini mwake au katika shajara yake, • kutumia ipasavyo msamiati aliojifunza katika sentensi, • kuandika mbinu za lugha (<i>k.v. methali, nahau, tashbihi na istiari</i>) alizopata katika matini aliyosoma na matumizi yake, • kutoa muhtasari wa ujumbe wa matini ya kujichagulia aliyoisoma na	1. Kusoma kwa mapana kuna umuhimu gani? 2. Je, unazingatia nini unapochagua matini ya kusoma?

			kuwasilisha kwa wenzake ili kupanua mawazo yao, kuweka rekodi ya aliyosoma kwa kuyanakili katika kijitabu au shajara yake kwa marejeleo ya baadaye.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapowasilisha kwa wenzake ujumbe wa matini aliyosoma. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapojichagulia matini ya kusoma na kutafuta maana ya msamiati kwenye kamusi. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusoma matini. - Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia msamiati aliojifunza. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapoeleza ujumbe kutokana na matini aliyosoma.				
Maadili: - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapochagua matini zifaazo na kuzisoma. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili vipengele vya kusoma kwa mapana. - Upendo: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake.				
Masuala Mtambuko: Suala la usalama: Mwanafunzi anaposoma matini kuhusu usalama wa sehemu za kazi.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
4.3 Kuandika	4.3.1 Uandishi Wa Kiuamilifu <i>Memo</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza maana ya memo ili kuipambanua, - kueleza umuhimu wa memo katika mawasiliano, - kujadili vipengele vya memo ili kuvibainisha, - kuandika memo kwa kuzingatia vipengele vyake, - kujenga mazoea ya kuandika memo akizingatia vipengele vyake.	Mwanafunzi aelekezwe: - kutumia kamusi au kifaa cha kidijitali kutafuta maana ya memo akiwa na mwenzake, - kuwasilisha maana ya memo katika vikundi, - kusoma vitabuni au kusakura mtandaoni kwa umakinifu umuhimu wa memo akishirikiana na wenzake, - kueleza umuhimu wa memo akishirikiana na wenzake, - kujadili vipengele vya memo (<i>ujumbe, muundo na mtindo</i>) akishirikiana na wenzake, - kutafiti vitabuni au kusakura mtandaoni ili kusoma vielelezo vya memo, - kuandika memo kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia vipengele vifaavyo na kuwasomea wenzake au kuwatumia kupitia kifaa cha kidijitali ili wamtotele maoni.	- Uandishi wa memo una umuhimu gani katika mawasiliano? - Tunazingatia mambo gani tunapoandika memo?

Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kusoma vielelezo vya memo. Pia, anapotumia kifaa cha kidijitali kuwatumia wenzake memo aliyoiandika ili waisome na kuitolea maoni. • Ubunifu: Mwanafunzi anapofaulu kuandika memo. • Kujiamini: Mwanafunzi anapofaulu kueleza umuhimu wa memo. • Uraia: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake wakitumia vifaa vya kidijitali kwa pamoja kusakura mtandaoni kuhusu umuhimu wa memo.
Maadili: • Heshima: Mwanafunzi anaposikiliza na kuthamini maoni ya wenzake. • Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali. • Upendo: Mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji. • Amani: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kujadili vipengele vya memo kwa utulivu.
Masuala Mtambuko: • Haki na majukumu ya kibinadamu: Mwanafunzi anapojifunza kuandika memo kuhusu majukumu mbalimbali ya kibinadamu kazini. • Usalama na ulinzi: Mwanafunzi anapojifunza kuandika memo kuhusu suala lengwa.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
4.4 Matumizi ya Lugha	4.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi <i>- tendatenda</i> <i>-tendeka</i> <i>-tendesha</i> <i>-tendana</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kujadili sifa bainifu za kauli ya kutendatenda, kutendeka, kutendesha na kutendana, b) kutambua vitenzi katika kauli ya kutendatenda, kutendeka, kutendesha na kutendana c) kutumia vitenzi katika kauli ya kutendatenda, kutendeka, kutendesha na kutendana ipasavyo katika sentensi,	Mwanafunzi aelekezwe: • kushirikiana na wenzake kujadili sifa bainifu za vitenzi katika kauli ya kutendatenda, kutendeka, kutendesha na kutendana (<i>k.m. kauli ya kutendeka hutumiwa kuonyesha kukamilika kwa kitendo au kurwa katika hali timilifu. Kauli hii hutumia viambishi -ek-, -ik-, -lek- na -lik-</i>), • kuteua vitenzi katika kauli ya kutendatenda, kutendeka, kutendesha na kutendana kwenye orodha ya maneno au katika sentensi akishirikiana na wenzake, • kugeuza vitenzi katika kauli ya kutenda hadi kauli ya kutendatenda, kutendeka, kutendesha na kutendana akishirikiana na wenzake, • kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kutendatenda, kutendeka, kutendesha na kutendana ipasavyo,	1. Je, ni kauli gani za vitenzi unazozijua? 2. Mnyambuliko wa vitenzi una umuhimu gani?

		d) kuchangamkia kutumia ipasavyo kauli ya kutendatenda, kutendeka, kutendesha, na kutendana ili kujenga ufasaha wa lugha.	kutunga sentensi au vifungu vifupi daftarinini au kwenye kifaa cha kidijitali akitumia vitenzi katika kauli ya kutendatenda, kutendeka, kutendesha na kutendana akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la usalama mahali pa kazi.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi kwa kutumia kauli lengwa katika sentensi. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kuandika sentensi katika kauli lengwa. - Ubunifu: Mwanafunzi anaponyambua vitenzi katika kauli lengwa. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapotambua kauli za vitenzi mbalimbali. - Kujiamini: Mwanafunzi anapoweza kutunga sentensi sahihi akitumia kauli lengwa.				
Maadili: - Amani: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kwa utulivu sifa bainifu za vitenzi katika kauli lengwa. - Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapogeza vitenzi katika kauli lengwa. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi za kugeza vitenzi katika kauli lengwa.				
Masuala Mtambuko: - Usalama mahali pa kazi: Mwanafunzi anapoandika sentensi akizingatia suala lengwa. - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kugeza vitenzi katika kauli ya kutendatenda, kutendeka, kutendesha na kutendana.				

5.0: KUKABILIANA NA MABADILIKO KATIKA FAMILIA

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
5.1 Kusikiliza na Kuzungumza	5.1.1 Kusikiliza kwa Kupambanua <i>Kusikiliza ili kutambua maana kutokana na msamiati, toni, viziada lugha na kiwango cha sauti</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kujadili vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa kupambanua ili kufasiri maana, - kujadili mielekeo kuhusu ujumbe kutokana na msamiati, toni, viziada lugha na kiwango cha sauti katika matini aliyosikiliza, - kuzingatia vipengele vifaavyo katika kusikiliza kwa kupambanua ili kufanikisha ufasiri wa ujumbe na maana, - kuchangamkia kushiriki katika usikilizaji wa kupambanua ili kukuza	Mwanafunzi aelekezwe: - kutafiti vitabuni au kwenye kifaa cha kidijitali kuhusu vipengele vya kusikiliza kwa kupambanua, - kujadili na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa kupambanua alivyovitafiti (<i>k.v. msamiati, toni, viziada lugha na kiwango cha sauti</i>), - kuandika kwenye chati vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa kupambanua walivyojadili na kuitundika ukutani kwa marejeleo ya baadaye, - kushiriki katika kusikiliza matini kuhusu suala lengwa kutoka kwa kifaa cha kidijitali ili kutambua mielekeo ya ujumbe na maana sahihi	- Je, kusikiliza kwa kupambanua kunasaidia vipi mawasiliano? - Utazingatia mambo gani katika kusikiliza kwa kupambanua ili kupata habari ipasavyo?

		stadi ya kusikiliza kwa ufasiri.	kutokana na msamiati, toni, viziada lugha na kiwango cha sauti akishirikiana na wenzake, • kuwasikiliza wenzake wakizungumza kwa kuzingatia msamiati, toni, viziada lugha, na kiwango cha sauti ili kupata ujumbe na maana na kuwatolea maoni.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya kuzingatia ili kufasiri maana katika matini aliyosikiliza. • Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapotambua ujumbe na maana katika matini kwa kuzingatia msamiati, toni, viziada lugha na kiwango cha sauti. • Kujiamini: Mwanafunzi anapowawasilishia wenzake vipengele vya kusikiliza kwa kupambanua alivyotafiti. • Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotafiti katika mtandao kuhusu vipengele vya kusikiliza kwa kupambanua.				
Maadili: • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili maana inayodokezwa na msamiati, toni, viziada lugha na kiwango cha sauti katika matini aliyosikiliza. • Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu mitazamo na mielekeo ya ujumbe katika matini aliyosikiliza. • Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika ujifunzaji.				

Masuala Mtambuko: • Mshikamano wa kijamii na utaifa: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kusikiliza matini kuhusu suala lengwa na kupambanua ujumbe na maana kutokana na msamiati, toni, viziada lugha, na kiwango cha sauti. • Suala la kukabiliana na mabadiliko: Mwanafunzi anaposhiriki katika kusikiliza matini inayohusu suala lengwa na kupambanua ujumbe na maana kutokana na msamiati, toni, viziada lugha, na kiwango cha sauti.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Mswali Dadisi Yalilopendekezwa
5.2 Kusoma	5.2.1 Kusoma kwa Kina <i>Usomaji wa kurashia</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kutambua namna mbalimbali za kurashia katika usomaji wa kina, b) kujadili umuhimu wa mbinu ya kurashia katika usomaji wa kina, c) kusoma matini kwa kurashia ili kupata ujumbe, d) kuthamini usomaji wa kina ili kukuza stadi ya kusoma.	Mwanafunzi aelekezwe: - kushirikiana na wenzake kueleza namna mbalimbali za kurashia (<i>k.v. kusoma mada, kusoma mada ndogo, kusoma utangulizi na hitimisho na kulenga maneno teule</i>), - kutafiti katika matini mbalimbali zikiwemo za mtandaoni umuhimu wa mbinu ya kurashia, - kurashia matini kuhusu kukabiliana na mabadiliko katika familia kwa kuzingatia ujumbe, - kuwasilisha ujumbe alioupata kwa kurashia ili wenzake wautolee maoni, - kutafiti matini zaidi katika mtandao salama na kuzisoma kwa kuzingatia mbinu ya kurashia.	- Usomaji wa kurashia unahusu nini? - Usomaji wa kurashia una umuhimu gani?
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kusoma matini kwa kuzingatia mbinu ya kurashia. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anaposoma matini lengwa kwa kina na kutambua ujumbe. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandao salama na kusoma kwa kuzingatia mbinu ya kurashia.				

Maadili: - Uwajibikaji: Mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu na kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji. - Amani: Mwanafunzi anaporidhia maoni ya wenzake katika mchakato wa ujifunzaji wa dhana ya kurashia.
Masuala Mtambuko: - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu kukabiliana na mabadiliko katika familia. - Suala la usalama: Mwanafunzi anaposakura mtandao salama kusoma matini mbalimbali.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
5.3 Kuandika	5.3.1 Uhariri: <i>Kuhariri Matini</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kufafanua umuhimu wa uhariri wa matini katika mawasiliano, b) kujadili changamoto zinazokumba uhariri wa matini, c) kufafanua mbinu za uhariri wa matini ili kuzipambanua, d) kuhariri matini akizingatia mtindo ufao wa uhariri, e) kujenga maarifa ya uhariri na kuyatumia kuboresha matini ili kufanikisha mawasiliano.	Mwanafunzi aelekezwe: • kutafiti vitabuni au mtandaoni umuhimu wa uhariri wa matini na kuufafanua akiwa na mwenzake, • kuwasilisha matokeo ya utafiti wake kwa wenzake ili wayatolee maoni kwa heshima, • kushirikiana na wenzake kujadili changamoto zinazokumba uhariri wa matini (<i>k.v. udumishaji wa lengo la mwandishi, uelewa wa muktadha na mada, maneno ya kiufundi au istilahi ngumu, usawazishaji wa matini na ubora wa matini</i>), • kuwasilisha changamoto alizojadili kwa wenzake ili wazitolee maoni, • kusakura mtandaoni mbinu za uhariri wa matini akiwa na wenzake,	1. Uhariri una umuhimu gani katika uandishi? 2. Tunazingatia mambo gani katika uhariri wa matini? 3. Je, mhariri hukumbana na changamoto gani anapohariri matini?

			- kufafanua mtindo ufao wa kuhariri matini kwa kuzingatia vipengele vya uhariri, - kushirikiana na wenzake kuhariri matini zikiwemo za mtandaoni akizingatia mtindo unaofaa wa uhariri, - kuwasilisha matini aliyohariri ili wenzake waitathmini na kuitolea maoni, - kusoma na kuhariri zaidi matini zilizochapishwa au za kidijitali kwa kuzingatia mtindo ufao wa uhariri.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapochangia kufanya uamuzi katika kikundi wanapotafiti mtandaoni na vitabuni kuhusu umuhimu wa uhariri wa matini. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu umuhimu wa uhariri wa matini akiwa na mwenzake. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anaposoma na kuhariri zaidi matini zilizochapishwa au za kidijitali kwa kuzingatia mtindo ufao wa uhariri. - Kujiamini: Mwanafunzi anapofaulu kuwasilisha makala aliyohariri ili wenzake waitathmini na kuitolea maoni. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anaposhiriki ipasavyo katika kujadili changamoto zinazokumba uhariri wa matini.				

Maadili:

- Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotolea maoni kazi ya wenzake wanapowasilisha makala waliyohariri.
- Uzalendo: Mwanafunzi anapoendeleza umoja na mshikamano katika vikundi wanapojadili changamoto zinazokumba uhariri wa matini.
- Heshima: Mwanafunzi anaposikiliza na kuthamini maoni ya wenzake wanapofafanua mtindo unaotumika kuhariri matini.

Masuala Mtambuko:

Suala la kukabiliana na mabadiliko: Mwanafunzi anapohariri makala kuhusu suala lengwa.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
5.4 Matumizi ya Lugha	5.4.1 Ukanushaji <i>Hali ya:</i> • -me- • hu- • -ka-	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya ukanushaji ili kuupambanua, b) kutambua viambishi vya ukanushaji wa hali ya -me-, hu- na -ka- katika matini, c) kukanusha sentensi kwa kuzingatia viambishi vya hali ya -me-, hu- na -ka- ili kufanikisha mawasiliano, d) kufurahia ukanushaji wa hali ya -me-, hu- na -ka- kwa mawasiliano bora.	Mwanafunzi aelekezwe: • kujadili maana ya ukanushaji ili kuupambanua akishirikiana na wenzake, • kutambua viambishi vya ukanushaji wa hali ya -me-, hu- na -ka- akiwa na mwenzake, • kusoma vitabuni au kusakura mtandaoni viambishi vya ukanushaji wa hali ya -me-, hu- na -ka- na kuwawasilishia wenzake ili watoe maoni, • kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia viambishi vya ukanushaji wa hali ya -me-, hu- na -ka- ipasavyo, • kukanusha sentensi kwa kuzingatia viambishi vya ukanushaji wa hali ya -me-, hu- na -ka- kwa kuzingatia	1. Ukanushaji hutumia viambishi gani? 2. Dhana ya ukanushaji inajitokeza vipi katika vitenzi?

			masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala lengwa.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni viambishi vya ukanushaji wa hali lengwa. • Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapokanusha sentensi ifaavyo. • Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anaposhiriki ipasavyo kukanusha sentensi kwa kutumia viambishi lengwa				
Maadili: • Uwajibikaji: Mwanafunzi anapochukua nafasi katika majadiliano kuhusu maana ya ukanushaji. • Heshima: Mwanafunzi anaposikiliza na kuthamini maoni ya wenzake katika shughuli za vikundi wanapokanusha sentensi katika hali lengwa. • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua viambishi vya ukanushaji wa hali lengwa.				
Masuala Mtambuko: • Suala la kukabiliana na mabadiliko: Mwanafunzi anapokanusha sentensi kuhusu suala lengwa. • Usalama mtandaoni: Mwanafunzi anaposakura mtandao salama kuhusu viambishi vya ukanushaji. • Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhiriki shughuli za kikundi.				

6.0: KUTUMIA TEKNOLOJIA KUDHIBITI TAKA

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
6.1 Kusikiliza na Kuzungumza	6.1.1 Uzungumzaji wa Papo kwa Hapo <i>Muktadha wa sherehe</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya uzungumzaji wa papo kwa hapo katika muktadha wa sherehe, b) kujadili miktadha ya sherehe ambapo uzungumzaji wa papo kwa hapo hutokea, c) kujadili umuhimu wa uzungumzaji wa papo kwa hapo katika muktadha wa sherehe, d) kujadili kanuni za uzungumzaji wa papo kwa hapo katika sherehe,	Mwanafunzi aelekezwe: • kueleza maana ya uzungumzaji wa papo kwa hapo katika muktadha wa sherehe, • kutafiti miktadha ya sherehe ambapo uzungumzaji wa papo kwa hapo hutokea, • kueleza wenzake matokeo ya utafiti wake kuhusu miktadha ya sherehe ambapo uzungumzaji wa papo kwa hapo hutokea (<i>k.v. harusini, kuadhimisha siku ya kuzaliwa, kuaga mtu au watu k.v. wanapomaliza shule, mtu anapostaafu au anapoenda ng'ambo</i>), • kujadili umuhimu wa uzungumzaji wa papo kwa hapo katika sherehe akishirikiana na wenzake,	1. Unaweza kuzingatia mambo gani ili kufanikisha uzungumzaji wa papo kwa hapo katika sherehe? 2. Uzungumzaji wa papo kwa hapo katika sherehe unachangia vipi katika mahusiano ya kijamii?

		e) kushiriki katika uzungumzaji wa papo kwa hapo katika sherehe akizingatia kanuni zifaazo, f) kufurahia kushiriki katika uzungumzaji wa papo kwa hapo katika miktadha ya sherehe katika jamii.	- kutafiti na kujadili kanuni za uzungumzaji wa papo kwa hapo katika sherehe (<i>kubaini aina ya sherehe, kuilenga hadhira, kudhihirisha ukakamavu, kutumia toni ifaayo, kuzingatia muundo/utaratibu ufaao, kutumia viziada lugha</i>) akishirikiana na wenzake, - kuigiza uzungumzaji wa papo kwa hapo katika sherehe kuhusu suala lengwa au masuala mengine ya kijamii akizingatia kanuni zifaazo ili wenzake wamtathmini, - kuwasikiliza wenzake darasani wakiwasilisha mazungumzo ya papo kwa hapo katika sherehe na kuwatolea maoni.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni kutafuta hoja kuhusu kanuni za uzungumzaji wa papo kwa hapo katika sherehe. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapojadili kanuni za uzungumzaji wa papo kwa hapo katika sherehe. - Kujiamini: Mwanafunzi anapofaulu kuigiza mazungumzo ya papo kwa hapo katika sherehe kwa kuzingatia kanuni zifaazo.				

Uraia: Mwanafunzi anapozingatia kanuni zifaazo za kudhibiti mawasiliano wakati anaposhirikiana na wenzake kujadili miktadha ambapo uzungumzaji wa papo kwa hapo hutokea kijamii.
Maadili: - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapozingatia hatua za kiusalama anaposakura mtandaoni na kupata habari kuhusu uzungumzaji wa papo kwa hapo katika sherehe. - Heshima: Mwanafunzi anaposikiliza na kuthamini maoni ya wenzake kuhusu kanuni za uzungumzaji wa papo kwa hapo katika sherehe. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa uzungumzaji wa papo kwa hapo katika sherehe.
Masuala Mtambuko: - Mahusiano ya kijamii: Mwanafunzi anapowasilisha mazungumzo ya papo kwa hapo katika sherehe kuhusiana na masuala ya kijamii. - Suala la teknolojia kwa maendeleo endelevu: Mwanafunzi anapowasilisha mazungumzo kuhusu nafasi ya teknolojia katika kudhibiti taka.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Swali Dadisi Lililopendekezwa
6.2 Kusoma	6.2.1 Kusoma kwa Ufasaha <i>Kifungu cha mjadala</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya kifungu cha mjadala ili kukibainisha, b) kujadili vipengele muhimu katika kusoma kifungu cha mjadala kwa ufasaha, c) kusoma kifungu cha mjadala akizingatia matamshi bora, d) kusoma kifungu cha mjadala akizingatia kasi ifaayo, e) kusoma kifungu cha mjadala akizingatia viakifishi, kiimbo na kiwango kifaacho cha sauti,	Mwanafunzi aelekezwe: - kutafiti vitabuni na mtandaoni kuhusu maana ya kifungu cha mjadala, - kujadili vipengele muhimu katika kusoma kifungu cha mjadala kwa ufasaha (<i>k.v. matamshi bora, kiwango cha sauti, kasi, kiimbo na viziada lugha vifaavyo</i>) akiwa na wenzake, - kutumia kifaa cha kidijitali kutazama na kusikiliza watu wanaosoma vifungu vya mjadala kwa ufasaha, - kusoma kifungu cha mjadala kwa ufasaha akizingatia vipengele vifaavyo vya kusoma kwa ufasaha ili kupata ujumbe mahususi, - kutumia kifaa cha kidijitali kwa uangalifu kusakura mtandaoni kifungu cha mjadala na kusoma kwa ufasaha,	Unazingatia mambo gani ili kuwasilisha ujumbe wa kifungu cha mjadala ipasavyo unaposoma?

		f) kusoma kifungu cha mjadala akizingatia viziada lugha, g) kujenga mazoea ya kusoma kifungu cha mjadala kwa ufasaha.	- kuwasomea wenzake kifungu cha mjadala kuhusu suala lengwa akizingatia vipengele vifaavyo vya kusoma kwa ufasaha ili wamtathmini na kumtolea maoni kwa heshima, - kutafiti vifungu zaidi vya mjadala kuhusu masuala mbalimbali, katika mtandao salama au vitabuni na kuvisoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposoma kifungu cha mjadala kwa ufasaha na kuwaeleza wenzake habari kutokana na kifungu alichosoma. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusakura mtandaoni kifungu cha mjadala na kusoma kwa ufasaha.				
Maadili: - Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake anaposhiriki shughuli za ujifunzaji. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotunza kifaa cha kidijitali anachokitumia katika shughuli za ujifunzaji.				
Masuala Mtambuko: Kuhifadhi mazingira: Mwanafunzi anaposoma kifungu cha mjadala kinachohusu suala lengwa la kudhibiti taka katika mazingira.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yanayopendekezwa
6.3 Kuandika	6.3.1 Uandishi wa Kiuamilifu <i>-Ripoti ya kawaida</i> <i>-Ripoti rasmi</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya ripoti ili kuipambanua, b) kujadili umuhimu wa ripoti katika mawasiliano, c) kueleza maana ya ripoti ya kawaida na ripoti rasmi ili kuibainisha, d) kujadili vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa ripoti ya kawaida na ripoti rasmi, e) kuandika ripoti ya kawaida na rasmi kwa kuzingatia vipengele vyake,	Mwanafunzi aelekezwe: - kushirikiana na wenzake kueleza maana ya ripoti, - kutafiti vitabuni au kwenye mtandao salama kuhusu umuhimu wa ripoti katika mawasiliano, - kuwasilisha matokeo ya utafiti kuhusu umuhimu wa ripoti katika mawasiliano kwa wenzake, - kushirikiana na wenzake kutafiti mtandaoni au vitabuni kuhusu maana ya ripoti ya kawaida na ripoti rasmi, - kushirikiana na wenzake kujadili vipengele vya kuzingatia katika kuandika ripoti ya kawaida na ripoti rasmi (<i>ujumbe na muundo</i>), - kuandika ripoti ya kawaida na rasmi (kuhusu suala lengwa au suala lolote linaloathiri jamii) akizingatia vipengele vyake,	- Ni vipengele vipi vya ripoti vinavyohakikisha taarifa inaeleweka ipasavyo? - Ni kwa jinsi gani uandishi wa ripoti sahihi huchangia maamuzi bora katika jamii?

		f) kujenga mazoea ya kuandika ripoti ili kurahisisha mawasiliano.	kuwasomea au kuwasambazia wenzake ripoti yake ili waitathmini na kuitolea maoni.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapoweka wazi hoja zake wakijadili maana ya ripoti. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni kuhusu ripoti ya kawaida na rasmi. Pia, anapoandika ripoti na kuwasambazia wenzake kupitia kifaa cha kidijitali. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapoandaa hoja za kuandikia ripoti kuhusu suala lengwa. - Kujiamini: Mwanafunzi anapofaulu kuandika ripoti na kuiwasilisha kwa wenzake.				
Maadili: - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotafiti vitabuni au kwenye mtandao salama umuhimu wa ripoti katika mawasiliano. - Heshima: Mwanafunzi anaposikiliza na kuthamini maoni ya wenzake katika kuwasilisha matokeo ya utafiti kuhusu umuhimu wa ripoti katika mawasiliano. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na kuwathamini wenzake wanapojadili vipengele vya kuzingatia katika kuandika ripoti.				
Masuala Mtambuko: - Usalama mtandaoni: Mwanafunzi anaposakura katika mtandao salama kupata maana ya ripoti ya kawaida na rasmi. - Kutumia teknolojia kudhibiti taka: Mwanafunzi anapoandika ripoti kuhusu suala lengwa.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Swali Dadisi Lililopendekezwa
6.4 Matumizi ya Lugha	6.4.1 Aina za Maneno <i>- Aina za vitenzi</i> <i>- Aina za vielezi</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kujadili aina za vitenzi na vielezi ili kuzifafanua, b) kutumia ipasavyo aina za vitenzi na vielezi katika matini, c) kufurahia matumizi ya aina za vitenzi na vielezi katika sentensi.	Mwanafunzi aelekezwe: • kusoma vitabuni au kusakura mtandaoni aina mbalimbali za vitenzi na vielezi akishirikiana na wenzake, • kutaja mifano ya aina mbalimbali za vitenzi na vielezi akishirikiana na wenzake, • kudondoa aina mbalimbali za vitenzi (<i>k.v. kikuu, kisaidizi na kishirikishi</i>) na vielezi (<i>k.v. mahali na wakati</i>) katika sentensi, • kujadili aina mbalimbali za vitenzi na vielezi akishirikiana na wenzake, • kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia aina mbalimbali za vitenzi na vielezi ipasavyo, • kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia aina za vitenzi na vielezi akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala lengwa na kuwawasilishia wenzake ili wamtotee maoni.	Ufahamu wa aina mbalimbali za maneno unachangia vipi mawasiliano?

Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutaja aina mbalimbali za vitenzi na vielezi. • Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapotunga sentensi kwa usahihi akitumia aina mbalimbali za vitenzi na vielezi. • Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura katika mtandao salama matumizi ya aina mbalimbali za vitenzi na vielezi.
Maadili: • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi akitumia aina mbalimbali za vitenzi na vielezi. • Heshima: Mwanafunzi anaposikiliza na kuthamini maoni ya wenzake wakieleza kuhusu aina mbalimbali za vitenzi na vielezi. • Amani: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutaja mifano ya aina mbalimbali za vitenzi na vielezi kwa utulivu.
Masuala Mtambuko: • Kutumia teknolojia kudhibiti taka: Mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa. • Usalama mtandaoni: Mwanafunzi anaposakura katika mtandao salama kupata matumizi ya aina mbalimbali za vitenzi na vielezi.

7.0: UADILIFU KATIKA UONGOZI WA KIJAMII

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
7.1 Kusikiliza na Kuzungumza	7.1.1 Kuzungumza kwa Ufasaha <i>Mjadala</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kutambua miktadha ambapo mjadala hutokea, b) kujadili kanuni za kuandaa mjadala ili kuzibainisha, c) kujadili kanuni za kufanikisha mjadala ili kuzibainisha, d) kushiriki mjadala kuhusu suala lengwa akizingatia kanuni za kufanikisha mjadala, e) kuonea fahari nafasi ya katika mjadala ili kukuza mawasiliano.	Mwanafunzi aelekezwe: • kutambua miktadha ambapo mjadala hutokea (<i>k.v. shuleni, bungeni, kwenye mabaraza, vituo vya utangazaji na mitandao ya kijamii</i>), • kujadili kanuni za kuandaa mjadala (<i>k.v. kutafiti kuhusu suala lengwa, kuifahamu hadhira lengwa ili kuteua mbinu zifaazo za kushawishi, kujua malengo ya mjadala</i>) akiwa na wenzake, • kushirikiana na wenzake kujadili kanuni za kufanikisha mjadala (<i>k.v. kusikiliza hoja za wengine kwa makini, kuzungumza kwa zamu, kutodharau mchango kutoka kwa upande wa upinzani, kutumia lugha ya heshima na ya kitaaluma, kudumisha nidhamu</i>	1. Kwa nini ni muhimu kuwa na kanuni za kufuata katika mjadala? 2. Je, kuwa na stadi za kushiriki mjadala maishani kuna faida gani?

57

			wakati wa kuzungumza, kuchukua msimamo kuanzia mwanzo, kuzingatia ukweli wa suala unalozungumzia, kuthibitisha hoja kwa kuzingatia ukweli usiopingika kuhusu suala husika, kutumia viziada lugha panapofaa, kutumia mbinu za lugha kama vile maswali ya balagha kuishawishi hadhira kukubaliana na mtazamo wako), • kusikiliza mjadala katika kifaa cha kidijitali na kubaini kanuni za kufanikisha mjadala zilizotumiwa akishirikiana na wenzake, • kufanya maandalizi ya mjadala kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake, • kushiriki mjadala na wenzake kuhusu masuala mbalimbali ya kitaifa, likiwemo suala la uadilifu katika uongozi wa kijamii, huku	
--	--	--	---	--

58

			akizingatia kanuni zifaazo za kufanikisha mjadala.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: ● Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kanuni za kuandaa na kufanikisha mjadala. ● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapowazia kanuni zifaazo za kuandaa na kufanikisha mjadala. ● Kujiamini: Mwanafunzi anapofanikiwa kuwashawishi wenzake kuhusu ukweli fulani wa suala lengwa. ● Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposikiliza mjadala katika kifaa cha kidijitali na kubaini kanuni zilizotumiwa. ● Uraia: Mwanafunzi anapotambua hisia za wengine kuhusu suala linalojadiliwa.				
Maadili: ● Heshima: Mwanafunzi anapowasikiliza wenzake katika mjadala na kuthamini maoni yao. ● Upendo: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanikisha mjadala kwa kujaliana. ● Uwajibikaji: Mwanafunzi anapochukua nafasi ya kuendeleza kikao cha mjadala na kudumisha nidhamu wakati wa mjadala. ● Uzalendo: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kuhusu suala lengwa. ● Uadilifu: Mwanafunzi anaposhiriki mjadala kuhusu suala la uadilifu katika uongozi wa kijamii.				
Masuala Mtambuko: ● Suala la uongozi: Mwanafunzi anaposhiriki mjadala kuhusu suala lengwa. ● Mshikamano wa kitaifa: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika mjadala na kuheshimu maoni yao.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
7.2 Kusoma	7.2.1 Kusoma kwa Ufahamu <i>Kifungu cha kupasha habari</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza ujumbe mahususi katika kifungu cha kupasha habari, - kupanga matukio yanavyofuatana katika kifungu cha kupasha habari, - kufanya utabiri na ufasiri wa ujumbe kutokana na kifungu cha kupasha habari, - kujadili maana ya msamiati katika kifungu cha kupasha habari na kuutumia ipasavyo katika sentensi, - kuchangamkia kusoma kifungu ili kukuza stadi za kusoma ufahamu.	Mwanafunzi aelekezwe: ● kusoma kifungu cha kupasha habari kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali, ● kueleza wenzake ujumbe mahususi ulio katika kifungu cha kupasha habari alichokisoma kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali, ● kujadili matukio yanavyofuatana katika kifungu cha kupasha habari alichokisoma akiwa na wenzake, ● kufanya utabiri na ufasiri kutokana na kifungu cha kupasha habari alichokisoma na awasilishe kwa wenzake ili wamtolee maoni kwa njia ya heshima na upendo, ● kutafuta maana ya msamiati katika kifungu cha kupasha habari alichokisoma na kujadili na wenzake, ● kutumia msamiati alioupata kwenye kifungu cha kupasha habari katika kutunga sentensi.	1. Kifungu cha kupasha habari kinahusu mambo gani? 2. Kusoma kifungu cha kupasha habari kuna umuhimu gani? 3. Ni vipengele vipi mwanafunzi anastahili kuzingatia ili kupata ujumbe katika kifungu cha kupasha habari?

Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: ● Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili jinsi matukio yanavyofuatana katika kifungu cha kupasha habari. ● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapohusika katika kutabiri na kufasiri ujumbe wa kifungu cha kupasha habari. ● Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposhiriki kusoma kifungu cha kupasha habari kutoka kwa kifaa cha kidijitali. ● Ubunifu: Mwanafunzi anapotumia msamiati ulio katika kifungu cha kupasha habari kutunga sentensi.
Maadili: ● Uwajibikaji: Mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika shughuli za ujifunzaji na wenzake. ● Heshima: Mwanafunzi anapotambua na kuthamini mchango wa wenzake katika shughuli za ujifunzaji. ● Uadilifu: Mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.
Masuala Mtambuko: ● Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposoma na kuwaeleza wenzake ujumbe kuhusiana na suala lengwa. ● Uongozi na utawala mwema: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili matukio yanavyofuatana kutoka kwa kifungu cha ufahamu kuhusiana na suala lengwa.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
7.3 Kuandika	7.3.1 Uandishi wa Kiuamilifu <i>Hotuba</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya hotuba ili kuipambanua, b) kujadili umuhimu wa hotuba katika mawasiliano, c) kujadili vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa hotuba ili kuvibainisha, d) kuandika hotuba akizingatia vipengele vya hotuba kikamilifu, e) kuchangamkia kuandika hotuba ili kufanikisha mawasiliano.	Mwanafunzi aelekezwe: ● kueleza maana ya hotuba ili kuipambanua akishirikiana na wenzake, ● kujadili umuhimu wa hotuba akishirikiana na wenzake, ● kutafiti vitabuni au katika mtandao salama vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa hotuba (<i>ujumbe, muundo na mtindo</i>), ● kujadili vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa hotuba akishirikiana na wenzake, ● kusoma au kusikiliza vielelezo vya hotuba kutoka vyombo vya kidijitali, ● kuandika hotuba kwa kuzingatia vipengele vya uandishi wa hotuba.	1. Uandishi bora wa hotuba una umuhimu gani? 2. Tunazingatia vipengele vipi tunapoandika hotuba?

Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapojadili na wenzake kuhusu vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa hotuba. • Ubunifu: Mwanafunzi anapofaulu kuandika hotuba kwa kuzingatia vipengele vya uandishi wa hotuba. • Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochangia katika mijadala kuhusu vipengele vya hotuba.
Maadili: • Uadilifu: Mwanafunzi anapoandika hotuba inayohusu suala lengwa. • Uzalendo: Mwanafunzi anaposoma au kusikiliza vielelezo vya hotuba kuhusu suala lengwa kutoka kwa vifaa vya kidijitali. • Haki za kijamii: Mwanafunzi anapoandika hotuba kuhusu suala lengwa.
Masuala Mtambuko: • Uadilifu: Mwanafunzi anapoandika hotuba kuhusu suala lengwa. • Kufanya maamuzi: Mwanafunzi anapochagua mada mbalimbali za kuandikia hotuba.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
7.4 Matumizi ya Lugha	7.4.1 Uundaji wa Maneno <i>-Nomino kutokana na kitenzi</i> <i>-Nomino kutokana na nomino</i> <i>-Nomino kutokana na kivumishi</i> <i>- Kivumishi kutokana na kitenzi</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kujadili umuhimu wa uundaji wa maneno katika kukuza mawasiliano, b) kujadili mbinu za uundaji wa nomino kutokana na kitenzi, nomino kutokana na nomino, nomino kutokana na kivumishi na kitenzi ili kuzibainisha, c) kuunda nomino kutokana na kitenzi, nomino kutokana na nomino, nomino kutokana na kivumishi na kitenzi,	Mwanafunzi aelekezwe: • kujadili umuhimu wa uundaji wa maneno akiwa na wenzake, • kushirikiana na wenzake kujadili mbinu za uundaji wa nomino kutokana na kitenzi, nomino kutokana na nomino, nomino kutokana na kivumishi na kitenzi, • kutafti vitabuni na katika mtandao salama ili kupata nomino zilizoundwa kutokana na vitenzi, nomino zilizoundwa kutokana na nomino, nomino zilizoundwa kutokana na vivumishi na vivumishi vilivyoundwa kutokana na vitenzi na kuwawasilishia wenzake ili watoe maoni, • kuunda nomino kutokana na kitenzi, nomino kutokana na nomino, nomino kutokana na kivumishi na kitenzi, • kutumia maneno aliyounda	1. Je, kujifunza mbinu za uundaji wa maneno kuna umuhimu gani katika mawasiliano? 2. Je, ni mbinu gani ambazo tunaweza kutumia kuunda maneno katika lugha?

		d) kuchangamkia uundaji wa maneno ili kujenga ufasaha wa lugha katika mawasiliano ya kila siku.	kutunga sentensi au vifungu vifupi akishirikiana na wenzake, ● kutathmini sentensi zilizotungwa na wenzake kwa upole.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: ● Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili mbinu za uundaji wa maneno. ● Kujiamini: Mwanafunzi anapotathmini sentensi zilizotungwa na wenzake kwa usahihi. ● Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapotafiti vitabuni na mtandaoni na kuwawasilishia wenzake kazi yake. ● Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia maneno aliyounda.				
Maadili: ● Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji wanapojadili umuhimu wa uundaji wa maneno. ● Heshima: Mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji huku akithamini maoni ya wenzake. ● Upendo: Mwanafunzi anapotathmini sentensi zilizoundwa na wenzake na kuwakosoa kwa upole.				
Masuala Mtambuko: ● Uadilifu katika uongozi shuleni: Mwanafunzi anapotunga sentensi au vifungu vifupi vinavyohusu suala lengwa. ● Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.				

8.0: UNYANYASAJI WA KIJINSIA

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
8.1 Kusikiliza na Kuzungumza	8.1.1 Kuzungumza kwa Kushawishi <i>Ushawishi kuhusu maadili katika jamii</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kutambua aina za uzungumzaji wa kushawishi, b) kujadili kanuni za uzungumzaji wa kushawishi ili kuzipambanua, c) kujadili miktadha ambapo uzungumzaji wa kushawishi kuhusu maadili katika jamii hufanyika, d) kuwasilisha matini ya kushawishi kuhusu maadili katika jamii akizingatia kanuni zifaazo za	Mwanafunzi aelekezwe: ● kutambua aina za uzungumzaji wa kushawishi (<i>k.v. mijadala, hotuba, matangazo ya kibiashara, mahubiri na kampeni za kistasia</i>) akishirikiana na wenzake, ● kujadili kanuni za uzungumzaji wa ushawishi (<i>k.v. kuangazia ujumbe maalum, kuzungumza kwa uwazi, kuzingatia ukweli wa suala, kutoa ithibati kwa hoja anazofafanua, kutumia lugha inayoathiri hisia za hadhira ili kuishawishi, kutumia lugha inayomjengea msikilizaji picha halisi ya suala analowasilisha, kutumia lugha inayojenga utangamano kati yake na</i>	1. Je, unatumia vipengele vipi ili kuwashawishi watu unapowazungumzia kuhusu suala fulani? 2. Je, kutumia lugha ya kushawishi kuna umuhimu gani katika kuwahamasisha watu kuhusu maadili katika jamii?

		uzungumzaji wa kushawishi, e) kuonea fahari uzungumzaji wa kushawishi katika miktadha mbalimbali ili kukuza stadi ya kushawishi.	<i>msikilizaji, kutumia lugha inayomfanya msikilizaji kuhisi kwamba hata yeye atafaidika kwa jambo linalozungumziwa, kutumia sauti thabiti na kakamavu, kubadilisha kiimbo kulingana na wazo analosisitiza, kutumia viziada lugha na kutazama hadhira)</i> akishirikiana na wenzake, • kusikiliza matini kutoka kwa mwalimu au kifaa cha kidijitali na kutambua kanuni za uzungumzaji wa kushawishi zilizotumiwa akishirikiana na wenzake, • kushirikiana na wenzake kujadili miktadha ambapo uzungumzaji wa kushawishi kuhusu maadili katika jamii hufanyika (<i>k.v. maabadini, shuleni na sherehe za arusi</i>), • kutazama video za watu wakishiriki uzungumzaji wa	
--	--	--	--	--

67

			kushawishi na kujadili jinsi wawasilishaji walivyotumia vipengele vya kushawishi, • kuzungumza kwa ufasaha kuhusu maadili katika jamii akizingatia kanuni za kushawishi, • kujirekodi katika kifaa cha kidijitali kwa uangalifu, akizungumza kwa ufasaha na kuzingatia kanuni za ushawishi kuhusu suala la maadili katika jamii, • kumwonyesha mwenzake, mzazi au mlezi video ya uzungumzaji wa kushawishi aliyorekodi ili ampe maoni yake.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua aina za uzungumzaji wa kushawishi na kujadili kanuni za uzungumzaji wa aina hiyo. • Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapojirekodi akizungumza na kumwonyesha mzazi au mlezi wake video ili amtolee maoni.				

68

• Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujirekodi akishiriki katika mazungumzo ya kushawishi kuhusu maadili katika jamii. • Kujiamini: Mwanafunzi anapofanikiwa kuwawasilisha wenzake matini shawishi kwa kuzingatia kanuni za uzungumzaji wa kushawishi. • Uraia: Mwanafunzi anapowasilisha matini ya kushawishi kuhusu maadili katika jamii.
Maadili: • Uwajibikaji: Mwanafunzi anapojitolea kufanya uzungumzaji wa kushawishi kwa ufasaha. Pia anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kuifunzia. • Heshima: Mwanafunzi anapowapa wenzake zamu ya kuzungumza katika shughuli za kikundi. • Upendo: Mwanafunzi anapowatolea wenzake maoni kwa upole na kujali hisia zao. • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika mazungumzo ya kushawishi.
Masuala Mtambuko: • Suala la kijinsia: Mwanafunzi anaposhiriki uzungumzaji wa kushawishi akizingatia suala lengwa. • Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuwasilisha matini kuhusu maadili katika jamii kwa kutumia vipengele vifaavyo vya uzungumzaji wa kushawishi. • Haki za kibinadamu: Mwanafunzi anaposhiriki uzungumzaji wa kushawishi kuhusu maadili katika jamii.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Swali Dadisi Lililopendekezwa
8.2 Kusoma	8.2.1 Ufupisho <i>Kifungu Shawishi</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kujadili vipengele vya kuzingatia katika kufupisha kifungu shawishi, b) kufupisha kifungu shawishi kwa kuzingatia vipengele vya ufupisho, c) kuchangamkia nafasi ya ufupisho katika mawasiliano.	Mwanafunzi aelekezwe: • kujadili na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kufupisha kifungu shawishi, • kujadili na wenzake jinsi wanavyoweza kutumia stadi za ufupisho maishani, • kusoma vifungu shawishi mbalimbali vilivyofupishwa ili kutambua namna vipengele vya ufupisho vilivyozingatiwa, • kusoma vifungu shawishi kuhusu unyanyasaji wa kijinsia na kuvifupisha kwa kuzingatia vipengele vya ufupisho, • kuwasilisha ufupisho wake darasani ili wenzake wautolee maoni, • kutolea maoni ufupisho wa wenzake kwa heshima na upendo.	Ufupisho wa habari una umuhimu gani katika mawasiliano?
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa ufupisho na jinsi wanavyoweza kutumia stadi za ufupisho maishani.				

● Kujiamini: Mwanafunzi anapofupisha kifungu shawishi kwa usahihi na kuwawasilishia wenzake. ● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapotafakari kuhusu hoja za kudondoa katika kifungu shawishi.
Maadili: ● Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji. ● Amani: Mwanafunzi anapojumuika na wenzake na kufanya kazi kwa kuelewana. ● Heshima: Mwanafunzi anapowatolea wenzake maoni.
Masuala Mtambuko: Suala la kijinsia: Mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Swali Dadisi Lililopendekezwa
8.3 Kuandika	8.3.1 Uandishi wa Kiubunifu <i>Masimulizi kutokana na methali</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya insha ya methali, b) kujadili ujumbe kutokana na insha ya methali, c) kufafanua matukio katika insha ya methali, d) kuandika insha ya methali akizingatia ujumbe, mtindo na muundo ipasavyo, e) kuchangamkia kuandika insha ya methali ili kukuza ubunifu.	Mwanafunzi aelekezwe: ● kujadili na wenzake na kueleza maana ya insha ya methali, ● kujadili ujumbe kutokana na insha ya methali akishirikiana na wenzake, ● kujadili maana na matumizi ya methali mbalimbali watakazotumia kuandikia insha, ● kueleza matukio katika insha ya methali, ● kujadili muundo wa insha ya methali akiwa na wenzake, ● kuandika insha ya methali akizingatia ujumbe, mtindo na muundo ufao, ● kuwasomea wenzake insha aliyoandika kutokana na methali ili waitolee maoni kwa heshima na upendo.	Tunazingatia nini tunapoandika insha za methali?

Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapochangia katika kujadili ujumbe kutokana na insha ya methali. • Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapotunga kisa kutokana na methali. • Kujiamini: Mwanafunzi anapofaulu kuandika na kuwasomea wenzake insha ya masimulizi kutokana na methali ili waitolee maoni.
Maadili: • Heshima: Mwanafunzi anaposikiliza na kuthamini maoni ya wenzake katika mijadala kundini. • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili muundo wa insha ya methali. • Upendo: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao katika mijadala.
Masuala Mtambuko: • Mahusiano ya kijamii: Mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa. • Unyanyasaji wa kijinsia: Mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Swali Dadisi Lililopendekezwa
8.4 Matumizi ya Lugha	8.4.1 Mahusiano ya Kimaana <i>Visawe vya:</i> • <i>nomino</i> • <i>vitenzi</i> • <i>vivumishi</i> • <i>vielezi</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kujadili maana ya visawe ili kuvipambanua, b) kutambua visawe vya nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi katika matini mbalimbali, c) kutumia visawe vya nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi katika matini ipasavyo, d) kufurahia matumizi yafaayo ya visawe vya nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi ili kufanikisha mawasiliano.	Mwanafunzi aelekezwe: • kushirikiana na wenzake kujadili maana ya visawe, • kutumia chati, kadi maneno, mti maneno, kamusi, vitabu vya marejeleo au mtandao salama kutambua visawe vya nomino (<i>k.v. mzazi-mvyele, magonjwa-maradhi na taabu-shida</i>), vitenzi (<i>k.v. huzunika-sononeka, afiki-kubali, na tesa-sumbua</i>), vivumishi (<i>k.v. baya-ovu, mrembo-mbeja na zuri-njema</i>), vielezi (<i>k.v. mno-sana, polepole-taratibu</i>) akishirikiana na wenzake, • kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia visawe vya nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi ipasavyo, • kuandika sentensi akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala lengwa akitumia visawe mbalimbali vya nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi kwenye chati na kuzitundika ukutani au kuhifadhi kwenye kifaa cha	Visawe vya maneno vina umuhimu gani katika mawasiliano?

			kidijitali na kuwasambazia wenzake ili wamtotee maoni, • kutathmini sentensi za wenzake na kuwatolea maoni kwa heshima.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapoungana na wenzake kujadili visawe vya nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi. • Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni kutafuta visawe vya nomino, vitenzi, vivumishi, na vielezi. • Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapojaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia visawe vya nomino, vitenzi, vivumishi, na vielezi ipasavyo. • Ubunifu: Mwanafunzi anapoandika sentensi akitumia visawe mbalimbali vya nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi. • Kujiamini: Mwanafunzi anapofaulu kutumia ipasavyo visawe vya nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi.				
Maadili: • Uwajibikaji: Mwanafunzi anaposakura mtandao salama na kutafiti kuhusu visawe vya nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi na kutunza vifaa vya kidijitali. • Heshima: Mwanafunzi anapotathmini sentensi za wenzake na kuwatolea maoni. • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili visawe vya nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi. • Upendo: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao katika mijadala kuhusu visawe vya nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi.				
Masuala Mtambuko: • Suala la kijinsia: Mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu suala lengwa. • Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anapotunga sentensi akizingatia suala lengwa na kuwasambazia wenzake ili wamtotee maoni.				

9.0: UTAMADUNI NA MSHIKAMANO WA KIJAMII

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
9.1 Kusikiliza na kuzungumza	9.1.1 Usikilizaji Husishi <i>Miktadha rasmi ya kazini</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kutambua miktadha rasmi ambapo usikilizaji husishi hufanyika, b) kujadili umuhimu wa usikilizaji husishi katika kujenga mahusiano ya kikazi, c) kujadili kanuni za kuzingatia katika usikilizaji husishi katika miktadha rasmi kazini ili kujenga mahusiano, d) kushiriki usikilizaji husishi katika miktadha rasmi ya kikazi kwa kuzingatia kanuni zifaa za kujenga mahusiano,	Mwanafunzi aelekezwe: • kutambua miktadha rasmi ambapo usikilizaji husishi hufanyika (<i>k.v., vikao vya utoaji nasaha, maabadini, shuleni, viwandani, na mahakamani</i>), • kushirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa usikilizaji husishi katika kujenga mahusiano ya kikazi, • kujadili kanuni za kuzingatia katika usikilizaji husishi katika miktadha rasmi ya kikazi (<i>k.v. kumtazama mzungumzaji ana kwa ana, kuepuka vizuizi vya usikilizaji, kuzingatia viziada lugha, kuwa na mtazamo wazi usio wa nafsi, kutomhukumu mzungumzaji, kuomba ufafanuzi wa ujumbe na</i>	1. Usikilizaji husishi una umuhimu gani katika miktadha rasmi ya kikazi? 2. Utatumia mbinu gani ili kufanikisha usikilizaji husishi katika miktadha rasmi wa kikazi?

		e) kufurahia kushiriki usikilizaji husishi katika miktadha rasmi kwa kuzingatia vipengele vifaavyo.	<i>kutafakari</i>) akishirikiana na wenzake, kushiriki usikilizaji husishi katika miktadha rasmi ya kikazi kwa kuzingatia kanuni zifaazo akishirikiana na wenzake.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kanuni za kuzingatia katika usikilizaji husishi katika miktadha rasmi. - Kujiamini: Mwanafunzi anapoweza kushiriki usikilizaji husishi katika miktadha rasmi ya kikazi kwa kuzingatia kanuni zifaazo. - Uraia: Mwanafunzi anaposhiriki usikilizaji husishi akizingatia kanuni zinazojenga mahusiano katika miktadha rasmi ya kikazi.				
Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua miktadha rasmi ambapo usikilizaji husishi hufanyika. - Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapojadili kuhusu kanuni za kuzingatia katika usikilizaji husishi katika miktadha rasmi ya kikazi. - Haki za kijamii: Mwanafunzi anapojifunza umuhimu wa usikilizaji husishi katika kujenga mahusiano ya kikazi.				
Masuala Mtambuko: - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhiriki usikilizaji husishi katika miktadha rasmi kuhusu suala lengwa. Pia anaposhiriki katika mazungumzo ya kujenga mahusiano. - Kudhibiti mitazamo hasi kuhusu tamaduni za jamii nyingine: Mwanafunzi anaposhiriki usikilizaji wa kujenga mahusiano.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendezwa
9.2 Kusoma	9.2.1 Kusoma kwa Mapana <i>Matini ya Kujichagulia</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kujadili vipengele mbalimbali vya kuzingatia katika kusoma kwa mapana, - kusoma matini ya kujichagulia akizingatia msamiati na matumizi ya lugha, - kuandika muhtasari wa ujumbe wa matini aliyoisoma, - kufurahia kusoma kwa mapana ili kujenga ufasaha wa lugha.	Mwanafunzi aelekezwe: - kujadili na wenzake vipengele vya kusoma kwa mapana (<i>kutambua msamiati, kutambua ujumbe na kuandika muhtasari wa matini</i>), - kutambua matini ya kujichagulia vitabuni au katika mtandao salama kuhusu masuala lengwa au suala lolote linaloathiri jamii na kuisoma, - kutumia kamusi kutafuta maana za maneno asiyoyajua, - kuandika msamiati aliojifunza na maana yake daftarinini mwake au katika shajara yake, - kuandika mbinu za lugha (<i>k.v. methali, nahau, misemo, tashbihi na istiari</i>) alizopata katika matini aliyosoma na matumizi yake, - kutoa muhtasari wa ujumbe wa matini ya kujichagulia aliyoisoma na kuwasilisha kwa wenzake ili kupanua mawazo yao,	- Kusoma kwa mapana kunachangia vipi katika mawasiliano? - Je, unazingatia nini unapochagua matini ya kusoma?

			kuweka rekodi ya aliyosoma kwa kuyanakili katika kijitabu au shajara yake kwa marejeleo ya baadaye.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapowasilisha kwa wenzake ujumbe wa matini aliyosoma. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapojichagulia matini ya kusoma, kuisoma na kutafuta maana ya msamiati kwenye kamusi. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotambua matini ya kujichagulia katika kifaa cha kidijitali na kuisoma. - Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia msamiati aliojifunza. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapotoa muhtasari wa ujumbe wa matini ya kujichagulia aliyosoma na kuwasilisha kwa wenzake ili kupanua mawazo yao.				
Maadili: - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapozingatia usalama wa mtandaoni anaposoma matini za kidijitali. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya kusoma kwa mapana. - Heshima: Mwanafunzi anapowaeleza wenzake ujumbe wa matini aliyosoma na kuthamini maoni yao. - Uzalendo: Mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa (utamaduni na mshikamano wa kijamii).				
Masuala Mtambuko: - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposoma matini kuhusu utamaduni na mshikamano wa kijamii. - Usalama Mtandaoni: Mwanafunzi anaposakura katika mtandao salama kuchagua matini ya kusoma.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
9.3 Kuandika	9.3.1 Uandishi wa Kiuamilifu <i>Insha fafanuzi kuhusu Chanzo na athari</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya insha fafanuzi kuhusu chanzo na athari ili kuibainisha, b) kujadili vipengele vya insha fafanuzi kuhusu chanzo na athari katika uandishi, c) kutambua hoja za kuandikia insha fafanuzi kuhusu chanzo na athari, d) kuandika insha fafanuzi kuhusu chanzo na athari akizingatia vipengele vyake, e) kufurahia kuandika insha fafanuzi ili kufanikisha mawasiliano.	Mwanafunzi aelekezwe: - kutafiti maana ya insha fafanuzi kuhusu chanzo na athari vitabuni na mtandaoni akishirikiana na wenzake, - kueleza maana ya insha fafanuzi kuhusu chanzo na athari, - kujadili vipengele vya insha fafanuzi (<i>k.v. maelezo ya kina kuhusu chanzo cha kitu au hali, na athari yake, uangavu, muundo, nafsi ya tatu, kutofungamana na mtazamo wa mwandishi</i>) akishirikiana na wenzake, - kuorodhesha hoja za kuandikia insha fafanuzi kuhusu chanzo na athari, - kuandaa mpangilio wa vidokezo vya insha fafanuzi kuhusu chanzo na athari akishirikiana na wenzake, - kuandika insha fafanuzi kitabuni au kwenye kifaa cha kidijitali	- Insha fafanuzi huwa na vipengele gani? - Kuna uhusiano gani kati ya chanzo na athari?

			inayohusu chanzo na athari akizingatia vipengele vyake, kuwasomea wenzake insha fafanuzi kuhusu chanzo na athari aliyoiandika au kuwasambazia ili waitolee maoni.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapoungana na wenzake kufafuta maana ya insha fafanuzi kuhusu chanzo na athari vitabuni na mtandaoni. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura kutafuta maana ya insha fafanuzi kuhusu chanzo na athari mtandaoni. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapotafakari na kuorodhesha hoja za kuandikia insha kuhusu chanzo na athari. - Kujiamini: Mwanafunzi anapofaulu kuandika insha fafanuzi inayohusu chanzo na athari akizingatia vipengele vyake.				
Maadili: - Heshima: Mwanafunzi anaposikiliza na kuthamini maoni ya wenzake katika mjadala kundini kuhusu vipengele vya insha fafanuzi kuhusu chanzo na athari. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandaa mpangilio wa vidokezo vya insha fafanuzi kuhusu chanzo na athari. - Upendo: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuthamini maoni yao kuhusu insha fafanuzi aliyoiandika.				
Masuala Mtambuko: Utatuzi wa migogoro kwa amani: Mwanafunzi anapotafuta namna ya kuafikiana na wenzake kunapozuka tofauti ya maoni baina yao.				

- Kujitambua: Mwanafunzi anaposhiriki ipasavyo kutoa hoja zake na anapofaulu kuzitumia kuandika insha ya ufafanuzi kuhusu suala lengwa. - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anapoandika insha kuhusu chanzo na athari kuhusu suala lengwa.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Swali Dadisi Lililopendekezwa
9.4 Matumizi ya Lugha	9.4.1 Sentensi <i>Sehemu za sentensi kwa kuzingatia:</i> - kiima - kiarifu - shamirisho - chagizo - kijalizo	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kujadili maana ya kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo na kijalizo katika sentensi ili kuzipambanua, - kujadili matumizi ya kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo na kijalizo katika sentensi ili kuzibainisha, - kujadili aina mbalimbali za shamirisho ili kuzibainisha, - kutunga sentensi kwa kutumia kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo na kijalizo ifaavyo, - kujenga mazoea ya kutumia kiima, kiarifu,	Mwanafunzi aelekezwe: - kujadili maana ya kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo na kijalizo katika sentensi akishirikiana na wenzake, - kujadili matumizi ya kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo na kijalizo katika sentensi akishirikiana na wenzake, - kusoma vitabuni au kusakura mtandaoni ili kutambua aina mbalimbali za shamirisho, - kujaza nafasi katika sentensi kwa kuzingatia kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo, na kijalizo ipasavyo, - kutunga sentensi kuhusu masuala mtambuko mbalimbali likiwemo	Kiima, kiarifu, shamirisho chagizo na kijalizo vina umuhimu gani katika sentensi?

		shamirisho, chagizo, na kijalizo katika mawasiliano.	suala lengwa ili kudhihirisha matumizi ya kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo, na kijalizo katika mawasiliano.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapotunga sentensi ili kudhihirisha matumizi ya kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo, na kijalizo ipasavyo. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni kuhusu aina mbalimbali za shamirisho. - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili matumizi ya kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo, na kijalizo katika sentensi. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anaposoma vitabuni au kusakura mtandaoni ili kutambua aina za shamirisho.				
Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili maana ya kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo, na kijalizo. - Heshima: Mwanafunzi anapothamini mchango wa wenzake wanapojadili matumizi ya kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo, na kijalizo katika sentensi. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotekeleza majukumu yake katika kujadili matumizi ya kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo na kijalizo.				
Masuala Mtambuko: - Utamaduni na mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anapoandika sentensi zinazohusu suala lengwa. - Usalama mtandaoni: Mwanafunzi anaposakura katika mtandao salama kuhusu aina mbalimbali za shamirisho.				

10.0: AFYA YA AKILI

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
10.1 Kusikiliza na Kuzungumza	10.1.1 Kusikiliza kwa Kuhakiki <i>Kuhakiki matini katika muktadha usio rasmi</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kutambua miktadha isiyo rasmi ambapo kusikiliza kwa kuhakiki hufanyika katika jamii, - kujadili kanuni za kusikiliza kwa kuhakiki matini katika muktadha usio rasmi, - kusikiliza mazungumzo katika muktadha usio rasmi kwa kuzingatia kanuni za kusikiliza kwa kuhakiki,	Mwanafunzi aelekezwe: - kushirikiana na wenzake kutambua miktadha isiyo rasmi ambapo kusikiliza kwa kuhakiki hufanyika katika jamii, - kutafiti kuhusu kanuni za kusikiliza kwa kuhakiki katika vitabu au mtandao salama akishirikiana na wenzake, - kushirikiana na wenzake kujadili kanuni za kusikiliza kwa kuhakiki matini katika muktadha usio rasmi, (k.v. kutambua tofauti kati ya hoja halisi na maoni ya kibinafsi, kuweza kupokea mawazo mapya kutegemea tafakuri na silika, kulinganisha mawazo mapya na ya awali, kuepuka mtazamo nafsi, kuepuka vizuizi vya usikilizaji, kutathmini bila kuhukumu, kuandika muhtasari wa hoja na	- Kusikiliza kwa kuhakiki katika muktadha usio rasmi kuna umuhimu gani? - Unaweza kutumia mbinu zipi ili kufanikisha kusikiliza kwa kuhakiki katika muktadha usio rasmi?

		d) kuhakiki matini aliyosikiliza katika muktadha usio rasmi, kwa kuzingatia vipengele vifaavyo, e) kufurahia kuhakiki matini ya kusikiliza kwa kutumia kanuni zifaazo katika mawasiliano ya kila siku.	<i>kudumisha maadili ya usikilizaji kama vile kumtazama mzungumzaji</i> akishirikiana na wenzake, - kuandika kanuni walizojadili kwenye chati na kuzitundika ukutani kwa marejeleo ya baadaye, - kutumia kanuni za kusikiliza kwa kuhakiki ili kuhakiki matini ya kusemwa kuhusu suala lengwa au suala jingine linaloathiri jamii, katika muktadha usio rasmi akizingatia vipengele vifaavyo (<i>k.v. ujumbe, wahusika na mitazamo ya wahusika kuhusu suala linalozungumziwa</i>), - kuandika tahakiki aliyofanya kwenye daftari lake au katika kifaa cha kidijitali, - kuwawasilishia wenzake tahakiki ya matini aliyosikiliza ili wamtolee maoni.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua miktadha isiyo rasmi ambapo kusikiliza kwa kuhakiki hufanyika katika jamii.				

- Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni kutafiti kuhusu kanuni za kusikiliza kwa kuhakiki. - Kujiamini: Mwanafunzi anapofaulu kutumia ipasavyo kanuni za kusikiliza kwa kuhakiki katika muktadha usio rasmi. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anaposoma katika vitabu au mtandaoni kuhusu kanuni za kusikiliza kwa kuhakiki akishirikiana na wenzake.
Maadili: - Uwajibikaji: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni na kupata habari kuhusu kusikiliza kwa kuhakiki. - Heshima: Mwanafunzi anapowatolea wenzake maoni kwa unyenyekevu kuhusu uhakiki wao. - Amani: Mwanafunzi anaposikiliza na kukubali tathmini ya wenzake kuhusu tahakiki yake. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kanuni za kusikiliza kwa kuhakiki. - Upendo: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa kuwajali na kuheshimu maoni yao kuhusu tahakiki yake.
Masuala Mtambuko: - Afya ya akili: Mwanafunzi anaposikiliza na kuhakiki matini kuhusu suala lengwa (afya ya akili). - Usalama mtandaoni: Mwanafunzi anaposakura mtandao salama ili kutafiti kuhusu kanuni za kusikiliza kwa kuhakiki. - Kujitambua: Mwanafunzi anapotambua uwezo wake katika kuhakiki matini ya kusikiliza kwa kuzingatia kanuni zifaazo.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Swali Dadisi Lililopendekezwa
10.2 Kusoma	10.2.1 Kusoma kwa Kina <i>Usomaji wa kuduhushi</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kujadili umuhimu wa kuduhushi katika usomaji wa kina, b) kujadili mambo ya kuzingatia katika kuduhushi matini, c) kusoma matini kwa kuduhushi kwa kuzingatia ufasiri wa mada, msamiati wa suala linalozungumziwa, matumizi ya lugha, maneno dokezi na kufasiri maana ya maneno hayo, d) kudondoa ujumbe mahususi katika matini aliyoisoma kwa kupitia mbinu ya kuduhushi,	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza umuhimu wa mbinu ya kuduhushi, - kutafiti katika matini mbalimbali zikiwemo za mtandaoni mambo ya kuzingatia katika kuduhushi matini (<i>k.v. kutafuta maneno makuu, maneno yaliyorudiwarudiwa na mifano</i>), - kusoma matini kuhusu suala lengwa au suala jingine linaloathiri jamii, kwa kutumia mbinu ya kuduhushi, akizingatia ufasiri wa mada, maneno dokezi na kufasiri maana ya maneno hayo, akiwa na wenzake - kushirikiana na wenzake kudondoa ujumbe mahususi katika matini aliyoisoma kwa kupitia mbinu ya kuduhushi, - kuwasilisha ujumbe aliyoupata kwa kuduhushi ili wenzake wautolee maoni, - kutafiti matini zaidi katika mtandao	Unawezaje kupata ujumbe katika matini kwa kutumia mbinu ya kuduhushi?

		e) kuthamini usomaji wa kina ili kukuza stadi ya kusoma.	salama na kuzisoma kwa kuzingatia mbinu ya kuduhushi.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kusoma kwa kuzingatia mbinu ya kuduhushi. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anaposoma matini lengwa akizingatia ufasiri wa mada, msamiati wa suala linalozungumziwa, matumizi ya lugha, maneno dokezi na ufasiri wa maana ya maneno hayo. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandao salama na kusoma kwa kuzingatia mbinu ya kuduhushi.				
Maadili: - Uwajibikaji: Mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu kutafiti matini zaidi katika mtandao salama na kuzisoma kwa kuzingatia mbinu ya kuduhushi. - Heshima: Mwanafunzi anapowaelewa na kuwathamini wenzake katika mchakato wa kuduhushi matini na kodondoa ujumbe mahususi.				
Masuala Mtambuko: - Afya ya akili: Mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa. - Usalama mtandaoni: Mwanafunzi anaposakura mtandao salama kusoma matini mbalimbali akitumia mbinu ya kuduhushi.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
10.3 Kuandika	10.3.1 Tafsiri	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kujadili aina mbalimbali za tafsiri ili kuzipambanua, b) kujadili vipengele vya kuzingatia katika kutafsiri matini andishi na matini semwa ili kuvibainisha, c) kufafanua sifa za mtafsiri bora wa matini andishi na matini semwa, d) kufanya tafsiri ya matini andishi na semwa kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya utafsiri,	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza dhana ya tafsiri akishirikiana na wenzake, - kutafiti vitabuni au katika mtandao salama aina mbalimbali za tafsiri (<i>k.v., neno kwa neno, sisisi, amilifu, tafsiri maana/kisemantiki na kimawasiliano</i>), - kujadili na wenzake aina za tafsiri alizozitafiti, - kutafiti vitabuni na mtandaoni kwa umakini fu kuhusu vipengele vya kuzingatia katika tafsiri andishi (<i>k.v. maandalizi, ufahamu wa lugha zinazohusika, ufahamu wa tamaduni, kuzingatia lengo la matini chanzi, uwazi, usahihi, uhalisia, uchambuzi, kusawidi rasimu na kudurusu</i>) na matini semwa (<i>k.v. kufahamu muktadha wa mazungumzo, kusikiliza kwa makini, kuweza kukumbuka kwa haraka maneno ya mzungumzaji, ufahamu wa tamaduni za hadhira, ufasaha wa lugha husika, viziada lugha vifaavyo</i>),	- Ni mambo yapi hurahisisha utafsiri wa matini? - Kuna uhusiano gani kati ya tafsiri ya matini andishi na matini semwa? - Kuelewa tamaduni za lugha chanzi na lugha lengwa kuna umuhimu gani kwa mfasiri?

		e) kufurahia kutafsiri ili kufanikisha mawasiliano.	- kujadili na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kutafsiri matini andishi na matini semwa alivyovitafiti, - kufafanua sifa za mtafsiri bora wa matini andishi (<i>k.v. umahiri wa lugha, ufahamu wa ujumbe, awe anaangazia mabadiliko ya kijamii, aelewe utamaduni wa jamii tofauti, uelewa wa lugha chanzi na mbunifu wa lugha</i>) na matini semwa (<i>k.v. ufahamu wa lugha chanzi na lugha lengwa, anayeweza kusikiliza kwa makini, uwezo wa kukumbuka, ukakamavu</i>) akishirikiana na wenzake, - kufanya tafsiri ya matini andishi na semwa kuhusu masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala lengwa kwa kuzingatia vipengele vya utafsiri, - kuwawasilishia wenzake tafsiri ya matini andishi na semwa alizofanya ili wazitolee maoni.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapojadili na wenzake aina mbalimbali za tafsiri. - Ubunifu: Mwanafunzi anapofaulu kufanya tafsiri kwa kuzingatia vipengele vya utafsiri.				

• Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anaposhiriki katika kutafiti vitabuni na mtandaoni kuhusu vipengele vya kuzingatia katika tafsiri.
Maadili: • Heshima: Mwanafunzi anaposhiriki mjadala kuhusu vipengele vya kuzingatia katika kutafsiri kifungu na kuthamini maoni ya wenzake. • Uwajibikaji: Mwanafunzi anapovitunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kutafiti kuhusu vipengele vya kuzingatia katika tafsiri. • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili aina mbalimbali za tafsiri.
Masuala Mtambuko: • Afya ya akili: Mwanafunzi anapofanya tafsiri kuhusu suala lengwa. • Wajibu wa kiraia: Mwanafunzi anapotafsiri makala mepesi yanayohusu sera za kiafya.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji	Swali Dadisi Lililopendekezwa
10.4 Matumizi ya Lugha	10.4.1 Isimujamii <i>Sajili za lugha:</i> • nyumbani • sokoni • usafiri • kituo cha polisi • mahakamani • bungeni • magazeti • vyombo vya habari • viwandani	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kujadili umuhimu wa sajili katika mawasiliano, b) kufafanua sifa za sajili ya nyumbani, sokoni, usafiri, kituo cha polisi, mahakamani, bungeni, magazeti, vyombo vya habari na viwandani ili kuzibainisha, c) kushiriki mazungumzo kwa kuzingatia sifa za sajili ya nyumbani, sokoni, usafiri, kituo cha polisi, mahakamani, bungeni, vyombo vya habari na viwandani ili kufanikisha mawasiliano, d) kujenga mazoea ya kuzingatia sifa zifaazo za matumizi ya lugha katika	Mwanafunzi aelekezwe: • kujadili dhana ya sajili na wenzake, • kufanya utafiti vitabuni au mtandaoni kuhusu umuhimu wa sajili za lugha katika jamii, • kushirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa sajili katika mawasiliano, • kufanya utafiti vitabuni au mtandaoni kuhusu sifa za kila sajili lengwa na kuwawasilishia wenzake darasani au akitumia kifaa cha kidijitali ili watoe maoni, • kutafiti katika mtandao salama vielelezo vya mazungumzo yanayozingatia sifa za sajili lengwa,	Kwa nini matumizi ya sajili tofauti ni muhimu katika mawasiliano ya kila siku?

		miktadha mbalimbali ili kufanikisha mawasiliano.	kushiriki mazungumzo na wenzake kwa kuzingatia sifa za sajili lengwa.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia wanapojadili dhana na kutafiti kuhusu sifa za sajili lengwa. - Kujiamini: Mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo ipasavyo kwa kuzingatia sifa za sajili. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapofanya utafiti kuhusu sifa za sajili lengwa vitabuni na mtandaoni. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo na wenzake kwa kuzingatia sifa za sajili mbalimbali.				
Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili umuhimu wa sajili katika mawasiliano. - Heshima: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili dhana na umuhimu wa sajili na kuthamini maoni ya wenzake. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji na kutunza vitabu na vifaa vya kidijitali. - Upendo: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa sajili na kuheshimu maoni yao. - Amani: Mwanafunzi anapokubali maoni ya wenzake kuhusu utafiti wake.				
Masuala Mtambuko: - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili dhana na umuhimu wa sajili. - Usalama mtandaoni: Mwanafunzi anapofanya utafiti katika mtandao salama kuhusu umuhimu na sifa za sajili lengwa. - Masuala mtambuko anuwai kulingana na sajili husika.				

MWONGOZO WA VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA

MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA				
Viwango Vigezo	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Kuweza kusikiliza na kutambua ujumbe na fani katika matini elezi (Kusikiliza kwa ufahamu)	Anatambua kwa wepesi ujumbe na fani katika matini elezi aliyosikiliza.	Anatambua ujumbe na fani katika matini elezi aliyosikiliza.	Anatambua sehemu ya ujumbe na fani katika matini elezi aliyosikiliza.	Anatambua sehemu ya ujumbe na fani katika matini elezi aliyosikiliza kwa kuongozwa.
Kuweza kusikiliza na kutamka sauti lengwa (Matamshi bora, sauti: /ch/, na /sh/, na /jw/ na /njw/)	Anasikiliza na kutamka sauti lengwa kwa ufasaha na ukakamavu.	Anasikiliza na kutamka sauti lengwa kwa ufasaha.	Anasikiliza na kutamka baadhi ya sauti lengwa.	Anasikiliza na kutambua baadhi ya sauti lengwa na kuzitamka akisaidiwa.

MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA				
Viwango Vigezo	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Kuweza kutoa maelezo sahihi, angavu na yenye mvuto kuhusu mahali, hali na vitu.	Anatoa maelezo sahihi, angavu na yenye mvuto kuhusu mahali, hali na vitu kwa utondoti.	Anatoa maelezo sahihi, angavu na yenye mvuto kuhusu mahali, hali na vitu.	Anatoa maelezo sahihi, angavu na yenye mvuto kuhusu baadhi ya mahali, hali na vitu kwa kiasi.	Anatoa maelezo sahihi, angavu na yenye mvuto kuhusu mahali, hali na vitu akisaidiwa.
Kuweza kusikiliza, kukumbuka ujumbe, kutoa maamuzi, maana, mielekeo na mitazamo kuhusu ujumbe katika matini aliyosikiliza.	Anasikiliza, kukumbuka ujumbe, kutoa maamuzi, maana, mielekeo na mitazamo kuhusu ujumbe katika matini aliyosikiliza kwa wepesi na ukakamavu.	Anasikiliza, kukumbuka ujumbe, kutoa maamuzi, maana, mielekeo na mitazamo kuhusu ujumbe katika matini aliyosikiliza.	Anasikiliza, kukumbuka ujumbe, kutoa maamuzi, maana, mielekeo na mitazamo kuhusu ujumbe katika matini aliyosikiliza kwa kiasi.	Anasikiliza, kukumbuka ujumbe, kutoa maamuzi, maana, mielekeo na mitazamo kuhusu ujumbe katika matini aliyosikiliza kwa kuauniwa.

MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA				
Viwango Vigezo	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Kuweza kuzungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia vipengele vya aina mbalimbali za uzungumzaji. (Mjadala, uzungumzaji wa kushawishi, uzungumzaji wa kupasha habari, uzungumzaji katika sherehe)	Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia vipengele vya aina mbalimbali za uzungumzaji kwa ubunifu.	Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia aina mbalimbali za uzungumzaji.	Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia baadhi ya vipengele vya aina mbalimbali za uzungumzaji.	Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia baadhi ya vipengele vya aina mbalimbali za uzungumzaji kwa kusaidiwa.

MADA: KUSOMA					
Vigezo	Viwango	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Kuweza kusoma kifungu cha simulizi kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha. <i>(Matamshi bora, kiwango kifaacho cha sauti, kasi ifaayo na ishara zifaazo)</i>	Anasoma kifungu cha simulizi kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha kwa ustadi.	Anasoma kifungu cha simulizi kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha.	Anasoma kifungu cha simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma kwa ufasaha.	Anasoma kifungu cha simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma kwa ufasaha kwa kuonyeshwa.	
Kuweza kusoma vifungu vya aina mbalimbali na kudondoa habari mahususi, kupanga matukio yanavyofuatana, kutabiri, kufasiri na kutumia msamiati ipasavyo. <i>(Kifungu cha ufahamu na simulizi)</i>	Anasoma vifungu vya aina mbalimbali na kudondoa habari mahususi, kupanga matukio yanavyofuatana, kutabiri, kufasiri na kutumia msamiati ipasavyo kwa wepesi na utondoti.	Anasoma vifungu vya aina mbalimbali na kudondoa habari mahususi, kupanga matukio yanavyofuatana, kutabiri, kufasiri, na kutumia msamiati ipasavyo.	Anasoma baadhi ya vifungu na kudondoa habari mahususi, kupanga matukio yanavyofuatana, kutabiri, kufasiri, na kutumia msamiati ipasavyo.	Anasoma baadhi ya vifungu na kudondoa habari mahususi, kupanga matukio yanavyofuatana, kutabiri, kufasiri na kutumia msamiati ipasavyo kwa kuelekezwa.	

MADA: KUSOMA				
Viwango Vigezo	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Kuweza kutambua vipengele vya ufupisho na kufupisha vifungu ipasavyo. <i>(Kifungu simulizi na kifungu shawishi)</i>	Anatambua vipengele vya ufupisho na kufupisha vifungu ipasavyo na kwa wepesi.	Anatambua vipengele vya ufupisho na kufupisha vifungu ipasavyo.	Anatambua baadhi ya vipengele vya ufupisho na kufupisha vifungu ipasavyo.	Anatambua baadhi ya vipengele vya ufupisho na kufupisha vifungu kwa kuongozwa.
Kuweza kusoma matini ya kujichagulia na kutambua ujumbe, msamiati, na matumizi ya lugha.	Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua ujumbe, msamiati, na matumizi ya lugha kwa mapana.	Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua ujumbe, msamiati, na matumizi ya lugha.	Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua kwa kiasi ujumbe, msamiati, na matumizi ya lugha.	Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua kwa kiasi ujumbe, msamiati, na matumizi ya lugha kwa kusaidiwa.
Kuweza kusoma matini kwa kurashia, kuduhushi, na kudondoa	Anasoma matini kwa kurashia, kuduhushi, na kudondoa ujumbe	Anasoma matini kwa kurashia, kuduhushi, na kudondoa ujumbe na	Anasoma matini kwa kurashia, kuduhushi, na kudondoa kwa kiasi	Anasoma matini kwa kurashia, kuduhushi, na kudondoa kwa kiasi ujumbe na matumizi ya

MADA: KUSOMA				
Viwango Vigezo	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
ujumbe na matumizi ya lugha ipasavyo (Usomaji wa kurashia na kudukusha)	na matumizi ya lugha ipasavyo kwa tafsili.	matumizi ya lugha ipasavyo.	ujumbe na matumizi ya lugha ipasavyo.	lugha ipasavyo kwa kuauniwa.

MADA: KUANDIKA				
Viwango Vigezo	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Kuweza kutumia alama ya kiulizi, alama hisi, ritifaa, semi koloni, na koloni ifaavyo.	Anatumia alama ya kiulizi, alama hisi, ritifaa, semi koloni, na koloni ifaavyo kwa wepesi.	Anatumia alama ya kiulizi, alama hisi, ritifaa, semi koloni, koloni ifaavyo.	Anatumia baadhi ya alama za kuakifisha ifaavyo.	Anatumia baadhi ya alama za kuakifisha kwa kusaidiwa.
Kuweza kuandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia vipengele	Anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia	Anaandika insha ya masimulizi kwa	Anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia baadhi ya	Anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia baadhi ya

MADA: KUANDIKA				
Viwango Vigezo	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
vifaavyo vya uandishi <i>(muundo, ujumbe, mtindo, na kanuni zifaazo za uandishi).</i>	vipengele vifaavyo vya uandishi kwa utondoti.	kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi.	vipengele vifaavyo vya uandishi.	vipengele vifaavyo vya uandishi kwa kuongozwa.
Kuweza kuandika aina mbalimbali za insha za kiuamilifu kwa kuzingatia vipengele vifaavyo. <i>(Barua rasmi, tawasifu, memo, ripoti, hotuba, insha fafanuzi- chanzo na athari).</i>	Anaandika aina mbalimbali za insha za kiuamilifu kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi kwa wepesi.	Anaandika aina mbalimbali za insha za kiuamilifu kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi.	Anaandika baadhi ya insha za kiuamilifu kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi.	Anaandika baadhi ya insha za kiuamilifu kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi kwa kuongozwa.
Kuweza kuhariri matini kwa kuzingatia vipengele vifaavyo. <i>(Kutambua na kudondoa makosa, kutathmini usahihi wa hoja, kurekebisha matumizi ya lugha na tahajia,</i>	Anahariri matini kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uhariri kwa wepesi.	Anahariri matini kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uhariri.	Anahariri matini kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uhariri.	Anahariri matini kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uhariri kwa kuelekezwa.

MADA: KUANDIKA				
Viwango Vigezo	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
<i>kutathmini matumizi ya viakifishi, kuzingatia kutumia mtindo ufaao).</i>				
Kuweza kufanya tafsiri ya kifungu kwa kuzingatia vipengele vya tafsiri <i>(maandalizi, ufahamu wa lugha zinazohusika, ufahamu wa tamaduni, kuzingatia lengo la matini chanzi, uwazi, usahihi, uhalisia, uchambuzi, kusawidi rasimu, kudurusu)</i>	Anafanya tafsiri ya kifungu kwa kuzingatia vipengele vya tafsiri kwa urahisi.	Anafanya tafsiri ya kifungu kwa kuzingatia vipengele vya tafsiri.	Anafanya tafsiri ya kifungu kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya tafsiri.	Anafanya tafsiri ya kifungu kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya tafsiri kwa kuongozwa.

MATUMIZI YA LUGHA					
Vigezo	Viwango	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Kuweza kutambua na kutumia aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili. <i>(Aina mbalimbali za nomino, vivumishi vitenzi, vielezi)</i>	Anatambua na kutumia aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili kwa uketo.	Anatambua na kutumia aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili.	Anatambua na kutumia baadhi ya aina za maneno katika lugha ya Kiswahili.	Anatambua na kutumia baadhi ya aina za maneno katika lugha ya Kiswahili kwa kuelekezwa.	
Kuweza kutambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi. <i>(Hali ya -me-, hu- na -ka-)</i>	Anatambua na kutumia viambishi vya hali katika vitenzi kwa wepesi.	Anatambua na kutumia viambishi vya hali katika vitenzi.	Anatambua na kutumia baadhi ya viambishi vya hali katika vitenzi.	Anatambua na kutumia baadhi ya viambishi vya hali katika vitenzi kwa kuelekezwa.	
Kuweza kutambua viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo. <i>(I-I, U-ZI, LI-YA, LI-LI, YA-YA)</i>	Anatambua viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo na kwa utondoti.	Anatambua viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo.	Anatambua baadhi ya viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo.	Anatambua baadhi ya viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia kwa kiasi upatanisho wa kisarufi ipasavyo.	

MATUMIZI YA LUGHA				
Viwango	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Kuweza kutambua visawe vya nomino, vitenzi na vivumishi na kuvitumia katika matini.	Anatambua visawe vya nomino, vitenzi na vivumishi na kuvitumia katika matini kwa ubunifu.	Anatambua visawe vya nomino, vitenzi na vivumishi na kuvitumia katika matini.	Anatambua visawe vya baadhi ya nomino, vitenzi, na vivumishi na kuvitumia katika matini.	Anatambua visawe vya baadhi ya nomino, vitenzi na vivumishi na kuvitumia katika matini kwa kusaidiwa.
Kuweza kutambua na kutumia kauli ya kutendeka, kutendesha, kutendatenda na kutendana katika vitenzi.	Anatambua na kutumia kauli ya kutendeka, kutendesha, kutendatenda, na kutendana katika vitenzi kwa uketo.	Anatambua na kutumia kauli ya kutendeka, kutendesha, kutendatenda na kutendana katika vitenzi.	Anatambua na kutumia baadhi ya kauli ya kutendeka, kutendesha, kutendatenda na kutendana katika vitenzi.	Anatambua na kutumia baadhi ya kauli ya kutendeka, kutendesha, kutendatenda na kutendana katika vitenzi kwa kuongozwa.
Kuweza kuunda maneno. <i>(Kuunda nomino kutokana na kitenzi, nomino kutokana na nomino, nomino kutokana na nomino)</i>	Anaweza kuunda nomino kutokana na kitenzi, nomino kutokana na nomino, nomino kutokana na kivumishi na kitenzi.	Anaweza kuunda nomino kutokana na kitenzi, nomino kutokana na nomino, nomino kutokana na nomino.	Anaweza kuunda baadhi ya nomino kutokana na kitenzi, nomino kutokana na nomino.	Anaweza kuunda baadhi ya nomino kutokana na kitenzi, nomino kutokana na nomino, nomino kutokana na nomino.

103

MATUMIZI YA LUGHA				
Viwango Vigezo	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
<i>na kivumishi na kivumishi kutokana na kitenzi).</i>	kivumishi kutokana na kitenzi kwa wepesi.	kivumishi na kivumishi kutokana na kitenzi.	na nomino, nomino kutokana na kivumishi na kivumishi kutokana na kitenzi.	kutokana na kivumishi na kivumishi kutokana na kitenzi kwa kusaidiwa.
Kuweza kujadili maana na kutumia sehemu za sentensi. <i>(Kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo na kijalizo)</i>	Anaweza kujadili maana na kutumia kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo na kijalizo katika sentensi kwa utondoti.	Anaweza kujadili maana na kutumia kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo na kijalizo katika sentensi.	Anaweza kujadili maana na kutumia kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo na kijalizo katika sentensi kwa kiasi.	Anaweza kujadili maana na kutumia kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo na kijalizo katika sentensi kwa kiasi, kwa kusaidiwa.
Kuweza kufafanua sifa za sajili za lugha. - nyumbani - sokoni - usafiri - kituo cha polisi - mahakamani - bungeni	Anaweza kufafanua sifa za sajili za lugha kwa wepesi na ukakamavu.	Anaweza kufafanua sifa za sajili za lugha.	Anaweza kufafanua baadhi ya sifa za sajili za lugha.	Anaweza kufafanua baadhi ya sifa za sajili za lugha kwa kuongozwa.

104

MATUMIZI YA LUGHA				
Vigezo	Viwango	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio
- magazeti - vyombo vya habari - viwandani				

MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI

Mada	Mapendekezo ya Mbinu za Kutathmini	Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia	Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji
Kusikiliza na Kuzungumza	a) Kumakinikia jinsi mwanafunzi anavyotumia lugha katika mawasiliano b) Kujibu maswali c) Maigizo d) Kutambua k.m. kwenye orodha e) Kuambatanisha maneno na majibu f) Mijadala g) Mazungumzo h) Matumizi ya ishara za mwili k.v. ishara za uso, za mikono na mabega kuimarisha masimulizi yake i) Wanafunzi kufanyiana tathmini	- Chati - Michoro na picha - Mgeni mwalikwa - Vifaa vya kidijitali (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video) - Mti maneno - Kapu maneno - Vitabu mbalimbali	1. Kazi ya vikundi 2. Vyama vya ushirika shuleni 3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali 4. Ziara za nyanjani 5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali
Kusoma	a) Kutunga sentensi k.m. kwa kutumia msamiati lengwa b) Kujibu maswali k.m. katika ufahamu c) Kutoa muhtasari wa ufahamu au matini yaliyosomwa d) Kusoma kwa sauti e) Wanafunzi kufanyiana tathmini f) Potifolio g) Shajara	- Tarakilishi/vipakatalishi - Kinasasauti - Rununu - Projekta - Kamusi mbalimbali	1. Kazi ya vikundi 2. Vyama vya ushirika shuleni 3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali 4. Ziara za nyanjani

Mada	Mapendekezo ya Mbinu za Kutathmini	Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia	Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji
			5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali
Kuandika	a) Kuandika tungo mbalimbali b) Wanafunzi kufanyiana tathmini c) Potifolio d) Shajara e) Mijadala kuhusu vidokezo vya insha	• Kielelezo cha insha ya masimulizi (methali) • Kielelezo cha memo • Kielelezo cha hotuba • Kielelezo cha insha fafanuzi • Kielelezo cha insha ya tawasifu • Kielelezo cha barua rasmi	1. Kazi ya vikundi 2. Vyama vya ushirika shuleni 3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali 4. Ziara za nyanjani 5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali
Sarufi	a) Kutambua k.m. kwenye orodha b) Kuambatanisha maneno lengwa c) Kujaza mapengo d) Kutunga sentensi e) Kazi mradi	• Tarakilishi/vipakatalishi • Kinasasauti • Rununu • Projekta • Kapu maneno • Mti maneno • Kadi maneno • Picha za vitu mbalimbali • Michoro • Chati	1. Kazi ya vikundi 2. Vyama vya ushirika shuleni 3. Ziara za nyanjani 4. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali

Mada	Mapendekezo ya Mbinu za Kutathmini	Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia	Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji
		• Mabango • Sanamu • Nyenzo halisi	